

# IKHILÂS NA TAQWÂ

## Usafi wa moyo na Uchamungu

**Othman Nuri TOPBASH**

ERKAM
PUBLICATIONS

**Istanbul - 2022**

© Kimechapwa na  Erkam  2022 / 1443 H

# IKHLÂS NA TAQWÂ

**USAFI WA MOYO NA UCHAMUNGU**

Othman Nuri Topbash

**Jina la Asili:** Îhlâs ve Takvâ
**Mwandishi:** Othman Nuri Topbash
**Msimamizi Mkuu:** Abdi Mohamed Adam
**Mfasiri:** Shuaıbu Kıfea
**Mhariri:** Ibrahimu H. Kabuga
**Msanifu jalada:** Altinoluk Graphics
**Kupangiliwa vizuri na:** Sarkhan Isgandarov
Nijat Garibov
**ISBN:** 978-9944-83-683-8
**Mchapaji:** Erkam Printhouse
**Anuani:** Ikitelli Organize Sanayi Bölgesi Mah. Atatürk Bulvarı, Haseyad 1. Kısım No: 60/3-C Başakşehir, Istanbul, Turkey
**Simu:** (+90-212) 671-0700 pbx
(+90-212) 671-0748
**Barua pepe:** info@islamicpublishing.org
**Tovuti:** www.islamicpublishing.org
**Language:** Swahili / Kiswahili

ERKAM PUBLICATIONS

# IKHLÂS NA TAQWÂ

## USAFI WA MOYO NA UCHAMUNGU

**Othman Nuri TOPBASH**

ERKAM
PUBLICATIONS

# YALIYOMO

## KHERI YA MOYO ULIOTAKASIKA:
## IKHILAS NA TAQWA-1

Maisha Ya Mtihani....15
Maisha Ya Taqwa....16
Moyo Wa Muungwana....19
Taqwa Hujumuisha Hatua Tatu....20
Kuweni Na Taqwa Katika Kila Jambo....21
Mwongozo Kwa Wale Wenye Taqwa....23
Kutafuta Njia Ya Kumfikia Yeye....24
Kwa Kumnyenyekea Mwenyezi Mungu....25

## KHERI YA MOYO ULIOTAKASIKA:
## IKHLAS NA TAQWA-II

Siri Ya Nusra (Wokovu)....27
Taqwa Katika Imani....28
Usiridhie Wala Kuuelekea Uovu....30

Kuweni Pamoja Na Wakweli ................................................32

Sawa Na Kushika Kaa La Moto............................................34

Taqwa Katika Ibada Hasahasa Swala ...................................35

Taqwa Katika Funga...........................................................36

Taqwa Katika Utoaji Wa Sadaka..........................................37

Taqwa Wakati Wa Hijja.......................................................39

Vikwazo Vitatu Vya Taqwa ................................................40

Taqwa Katika Mwenendo....................................................41

Hali Ya Kujali Zaidi Wengine (Îthaar) .................................42

Taqwa Katika Ihsaan (Wema)..............................................44

**KHERI YA MOYO ULIOTAKASIKA:**

**IKHLÂS NA TAQWÂ-III**

Taqwa Katika Kuridhia (Rida)..............................................47

Kheri Iko Kwa Mwenyezi Mungu Tu ..................................50

Taqwa Katika Kuomba Maghfira (Msamaha) Na Toba.......53

Kuamrisha Mema Na Kukataza Mabaya ..............................55

Taqwa Katika Kazi Ya Kuutumikia Uislamu (Khidma).......56

Taqwa Katika Uaminifu.......................................................59

Taqwa Katika Mapenzi Na Mahaba .....................................61

**NEEMA YA MOYO ULIOTAKASIKA:**

**IKHILAS NA TAQWA-IV**

Taqwa Katika Usafi Wa Moyo (Ikhlas) .................................65

Taqwa Katika Mali, Uhai Na Watoto ....................................66

Taqwa Katika Kutunza Amana .............................................67

Taqwa Katika Uwajibikaji......................................................69

Njia Pekee Ni Taqwa .............................................................70

Ubora Wa Taqwa ..................................................................71

Dalili Ya Taqwa .....................................................................71

Hii Ndiyo Taqwa! ..................................................................72

Jua La Taqwa ........................................................................72

"Mwenyezi Mungu Akujaalie Taqwa"...................................72

Mtihani Wa Taqwa ...............................................................73

Vazi La Taqwa ......................................................................74

Masurufu Ya Taqwa..............................................................75

# NENO LA AWALI

Shukurani na Sifa zote njema Anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye ameumba umbile la ulimwengu na kumweka mwanadamu kileleni mwa sanaa Yake hiyo, pia Akamfunulia wahyi kumpa Ujuzi, Ikhilaswi na Taqwa.

Swala na Salamu zimshukie Nabii Muhammad (s.a.w) ambaye ndiye njia ya ulimwengu, nuru ya upendo, mwangaza wa uwongofu na nyota ya jaha, yeye ndiye kigezo kikuu cha Ikhilaswi na Taqwa.

Maisha ya mwanadamu daima hutumika kwa namna moja au nyingine. Jambo muhimu ni jinsi gani yatumike, ama yatumike katika uchaMungu na yawe ya ikhilaswi Kwake au yatumike katika ujahili na yasiwe na maana yoyote.

Mambo muhimu zaidi yanayofanya maisha ya mtu yawe na maana ni taqwa (uchamungu) na usafi wa moyo (ikhilas). Taqwa ni kule kuyadhibiti matamanio ya kimwili na kuimarisha nguvu ya kiroho kwa njia ya swala za kumuelekea Mwenyezi Mungu na kuwatendea wema binadamu. Hivyo basi, taqwa huhitajika katika kila eneo la maisha, katika imani zetu, ibada zetu, mahusiano yetu na wengine, na hata katika kila pumzi ya uhai wetu.

Kuwa na taqwa maana yake ni kuwa rafiki wa Mwenyezi-Mungu, kuwa na moyo wenye siha ya imani hapa duniani, moyo ambao unaweza kuzingatia mafunzo yatokanayo na ishara za uweza wa Mwenyezi Mungu ulimwenguni, na kuwa na buruhani ya kuingia Peponi kwa rehema za Mwenyezi Mungu.

Kwa maneno mengine, kuwa na ikhilas na taqwa maana yake ni kuutakasa ulimwengu wetu wa ndani ya roho na aina zote za maradhi ya kiroho, kuziwezesha nyoyo zetu kufurahia Swala zetu na vitendo vyetu vinavyoendana na vile Atakavyo Mwenyezi Mungu. Hali hiyo ya moyo inaelezewa katika aya ifuatayo ya Qur'an: "Kwa hakika amefaulu aliyeitakasa nafsi yake," (Ala, 87:14).

Kuwa na ikhilaswi na taqwa maana yake ni kufungamana na MwenyeziMungu ndani ya moyo, hiyo ni kujipamba kwa sifa nzuri (Jamal) za MwenyeziMungu kama vile huruma, usamehevu, upole katika kuadhibu na kadhalika. Hii ina maana ya kutafuta radhi za MwenyeziMungu katika vitendo vyetu vyote na kwa pumzi zetu zote.

Hapana shaka kuwa ili kufikia daraja hilo mtu anahitajika kufanya jihadi ya kuubadili moyo wake. Mwenyezi Mungu anaufafanua ugumu wa jihadi hii ya nafsi kwa kuviapia viumbe vinne vya ulimwengu huu, baada ya hapo, anatwambia kuwa ni wale tu wazitakasao nyoyo zao ndio watakaonusurika:

"Naapa kwa jua na kwa mwangaza wake; Na kwa mwezi unapoliandama; Na kwa mchana unapolidhihirisha; Na kwa usiku unapolifunika; Na kwa mbingu na kwa Aliyezijenga; Na kwa ardhi na kwa Aliyeitandaza, Na kwa nafsi (roho) na kwa Aliyeitengeneza, Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake; Bila shaka amefaulu aliyeitakasa (nafsi yake), Na bila shaka amejihasiri aliyeifisha (nafsi yake)." (91:1-10).

Kama zinavyobainisha aya hizi, mwanadamu, kwa upande mmoja wa nafsi yake, anayo matamanio ya nafsi na ya kinyama, na kwa upande mwingine, anazo hisia za taqwa za kumkinga na nafsi yake mwenyewe. Kwa upande mmoja,ipo nafsi inayotaka kucheza matopeni, na kwa upande mwingine, ipo roho inayotaka kuelea mawinguni.

Rumi kaelezea jambo hili kwa tamathali ifuatayo:

"Ewe msafiri wa kweli! Ukitaka kuujua ukweli halisi, basi hajafa Firauni wala Musa, wote wawili wanaishi mwilini mwako, wakifichikana ndani ya uhai wako. Wanaendelea na vita yao ndani ya moyo wako. Ndiyo kusema basi unahitaji kuwatafuta mahasimu hawa wawili ndani ya nafsi yako."

Abu Dharr (r.a) kasimulia Hadith ifuatayo kutoka kwa Mtume (s.a.w):

Siku moja Mtume (saw) alisema: "Naijua aya moja: Laiti watu wangeishi kwa mujibu wa aya hii, basi ingelitosha (kuwa nusura yao).

Maswahaba wakauliza ni aya gani hiyo, naye akajibu:

"Na anayemwogopa Mwenyezi Mungu, Yeye Mwenyezi Mungu humtengenezea njia ya kuokoka. (Talaq, 65:2) (Ibn Majah, Zuhd, 24).

Siku moja mtu mmoja alikuja kwa Mtume (saw) na kuuliza:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi ninakwenda safarini, naomba uniombee dua."

Mtume akasema:

"Mwenyezi Mungu akupe taqwa!"

Mtu huyo akaomba dua zaidi kutoka kwa Mtume, naye Mtume akaendelea:

"Mwenyezi Mungu akusamehe dhambi zako"

Swahaba huyo akasema: Mama yangu na baba yangu watolewe muhanga kwa ajili yako ewe Mtume wa Mwenyezi-Mungu, naomba uniombee zaidi:

"MwenyeziMungu akujaalie wepesi popote utendapo

wema" Mtume alisema hivyo kujibu ombi hilo. (Tirmidhi, 44:3444).

Msingi wa dua ya Mtume kwa Swahaba huyo aliyekuwa mbioni kusafiri ulikuwa ni kumuombea taqwa kwanza na halafu msamaha wa dhambi zake na mwisho wepesi katika kufanya mema wakati wote na popote pale. Aliitaja taqwa kwanza kwani kwayo ndipo dhambi za mtu zinapoweza kusamehewa na matendo mema kufanyika kwa wepesi.

Ili kupata taqwa yatubidi tuishi maisha ya kutafakari na kutia mambo akilini. Mwenyezi Mungu anauliza katika Qur'an, akitukumbusha ujumbe wa Mtume na wa Mitume waliotangulia:

"Je hamufikiri?" (Hud, 11:30)

"Basi hamyatii akilini." (Hud 11:51), "basi je hamfahamu?" (Muminun, 23:80).

Mwanadamu anapopata upeo wa mbali wa kufikiri, huwa ni mtu wa kujiuliza-uliza muda wote: "Kwa nini nilikuja hapa duniani? Kwa nini naishi? Huu ulimwengu ninaoishi ni wa nani? Ni nani anayenipa riziki yangu?"

Pindi anapoanza kujiuliza maswali hayo, huwa hawi tena mtu wa kupoteza hata sekunde moja katika kumtumikia MwenyeziMungu. Ingawaje maisha yenyewe ni mafupi, bado mtu huwa na wasaa mwingi. Akitutahadharisha juu ya hili, Mtume (saw) amesema: "Kuna neema mbili ambazo watu huzipoteza: (nazo ni) Afya na Wasaa wa kufanya mema." (Bukhari, riqaq, 1).

Tukivuta picha ya mazingira magumu ya Siku ya Hesabu, hatutakuwa na hata sekunde moja ya kupoteza kwa kila dakika ya wasaa tuupatao kujiandaa na Akhera. Hivyo, ni muhimu

sana kuzingatia waadhi wa hapo juu pamoja na mauidha mengine ya Qur'an. Hapo tu ndipo dunia hii inapoweza kuwa bustani yenye mavuno katika maisha ya Akhera. Aya ifuatayo inabainisha ukweli huo:

"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu; na kila mtu aangalie anayoyatanguliza kwa ajili ya kesho (Akhera) na Mcheni Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu anazo habari za yote mnayoyatenda." (Hashr, 59:18).

Jambo la pili katika kufaulu kuipata taqwa ni kumjua Mtume (saw) na kuyafahamu maisha yake. Maswahaba walijua kuwa Mtume aliletwa kama rehema kwa walimwengu wote na wakampenda kuliko kitu chochote kile ikiwa ni pamoja na maisha yao. Waliiga kigezo chake katika kila jambo. Mbali ya hivyo, walikiheshimu kama neema kila kilichohusiana naye. Hadith ifuatayo inabainisha kuwa Mtume mwenyewe aliridhia jambo hili:

Anas bin Malik (ra) kasimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, mara nyingi, alitembelea nyumbani kwa Umm Sulaym (ambaye alikuwa ni dada wa mamake wa kunyonya) na akalala hapo wakati mama huyo akiwa hayupo. Siku moja Mtume alilala nyumbani kwa mama huyo. Mwenyewe alipokuja, akaambiwa: nyumbani mwako yumo Mtume wa MwenyeziMungu kalala. Akaingia na kumkuta Mtume akivuja jasho ambapo jasho lilimwagikia kitambaa cha ngozi kilichotandikwa kitandani kwake. Akafungua mkoba wake wa manukato na kuanza kuzijaza chupa manukato hayo. Mtume (saw) alishituka na kuamka, na akauliza: Unafanya nini ewe Umm Sulaym? Akajibu: Ewe Mtume wa MwenyeziMungu, twawatafutia wanetu baraka kwa njia hii. Hapo Mtume akasema: umefanya jambo sahihi.

Hicho ndicho kiwango cha mapenzi walichokuwa na-

cho kwa Mtume (saw). Katika njia ya uwongofu, mafanikio makubwa ni yale ya kuishi maisha yaleyale ya imani aliyoishi Mtume (saw). Ni kwa kuishi hivyo tu ndipo imani, tabia na uadilifu wetu vitakapotengemaa. Kwa sababu hiyo, siku zote tuishi kwa kujiuliza swali hili:

"Je maisha yangu yanalingana na yale ya Mtume?"

Tujiulize swali hili katika kila eneo la maisha na katika kila jambo jipya linalojitokeza kwetu. Kitabu hiki chepesi ni mkusanyiko wa makala nilizoandika mimi mwenyewe katika jarida la Yuzuki, litokalo kila mwezi kwa lugha ya Kituruki, ambapo tulijaribu kwenda pamoja na wasomaji kuhusiana na jinsi gani taqwa inavyoweza kuingizwa vitendoni katika nyanja mbalimbali za maisha.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu aijaalie kazi hii iwe sadaka endelevu (swadaqat-i- jariya) kwa wale waliosaidia kuiandaa. Tunamuomba MwenyeziMungu alipe nguvu yenye athari kila neno lililosemwa na kila mstari ulioandikwa kwa minajili ya haki.

**Ewe Mola wangu! Tujaalie hisa katika maisha ya Mtume (saw) katika maisha yetu yote. Tuwezeshe kufikia kilele cha imani na utambuzi, tuutumikie ulimwengu mzima kwa mapenzi. Tuwezeshe kufikia peo za mbali za tafakuri, na tujaalie tuwe watu waliotengenea. Tuwezeshe kufaulu kuishi maisha ya taqwa na ikhilaswi bila kupoteza hata dakika moja.**

**Amin!**

**Othman Nuri Topbash**
4.7.2009
Istanbul, Uskudar

# Kheri ya Moyo Uliotakasika: *Ikhilas na Taqwa-1*

## MAISHA YA MTIHANI

Miongoni mwa mamilioni chungutele ya viumbe hai, binadamu ndiye ambaye Mwenyezi Mungu kamteua awe mwakilishi wa uzuri na utengenefu. Kamuumba kiumbe huyu mwenye utukufu mkubwa kwa umbile bora kabisa (*ahsan taqwim*), akampamba kwa sifa nyingi, ikiwa ni pamoja na maarifa, akili na ufahamu, na akamjaalia vipawa vingi. Kisha Mwenyezi Mungu akamleta mtu duniani kwa mtihani wa muda.

Hivyo, kuanzia kipindi cha mtu wa kwanza, Adam, hadi hivi sasa, sababu ya kiumbe huyu bora kuletwa duniani ni kutahiniwa. Kila mtu ambaye amekuja hapa duniani, amepita katika mtihani huo na akaondoka na kile alichostahili, sasa ni zamu yetu ambapo na sisi tunapita katika mtihani uleule kama wale waliotutangulia.

Tusighafilike kuwa katika kipindi chote cha historia, muundo wa mtihani huo umekuwa ni uleule mmoja: je mwanadamu anatumiaje akili yake, maarifa yake na ufahamu wake, vyote vikielekea kote kuwili; kwema na kuovu.

Jukumu la kwanza la mwanadamu ni kufaulu majaribio yote anayokumbana nayo ndani ya chumba cha mtihani huu mkubwa ambacho ni dunia na kwa kupitia majaribio hayo, apate kuwa mja mwema wa MwenyeziMungu.

Katika mtihani huu mkubwa, MwenyeziMungu, Mwingi wa Rehema hakutuacha hivi hivi bila mwongozo. Ameshusha wahyi wenye maneno yaliyozama ndani kabisa ili kutuongoza na kutusaidia kupata mafanikio hapa duniani. Kaiteremsha Qur'an, kiongozi sahihi cha imani, ikiwa ni neema kwa walimwengu.

Vilevile kawatuma Manabii, walimu wakubwa wa mwanadamu, kama ishara ya rehema, waje kutufikishia na kutufafanulia ujumbe wa MwenyeziMungu. Aidha katujaalia neema mahususi ya nyongeza ambayo ni ile ya kuwa wafuasi wa umma wa Muhammad (*Ummah*).

Hivyo basi, kupata mafanikio katika dunia hii ya mitihani huku tukimhimidi Mola wetu ndilo jambo muhimu zaidi. Kwa hakika njia pekee ya kupata mafanikio ni ile ya kuhiyari kuishi maisha haya kwa kufuata njia iliyoainishwa katika ufunuo wa mwisho wa MwenyeziMungu, nao ni Qur'an Tukufu.

## MAISHA YA TAQWA

Undani na maana ya maisha vinakutikana ndani ya taqwa ambapo kuishi maisha ya taqwa, kimsingi, kuna maana ya kuwa rafiki wa kweli wa MwenyeziMungu, kuifikia Pepo na kuwa na moyo wa kuweza kuelewa kwa undani kabisa neema za MwenyeziMungu. Hivyo, ukweli wa taqwa ni kwamba mtu apate nafsi iliyotakasika na uovu kabisa-kabisa na kumuelekea Mola wake kwa imani thabiti; hii ndiyo njia pekee ambayo kwayo mtu huweza kumfikia Mwenyezi Mungu.

Taqwa ndilo jambo muhimu la kuleta furaha katika maisha haya na maisha ya Akhera, ambapo MwenyeziMungu kaitaja taqwa katika jumla ya aya mia mbili na hamsini na nane akitoa maelekezo mengi ya jinsi ya kuifikia taqwa. Kwa kifupi, Mwenyezi Mungu anatutaka tuwe na taqwa katika kila hatua ya maisha, katika imani na vitendo vyetu, kwa kila pumzi tunayovuta.

***Taqwa ni Nini?***

Marafiki wa MwenyeziMungu wameielezea taqwa kwa namna mbalimbali. Maana ya kikamusi ya taqwa ni mwepuko, kinga au ulinzi dhidi ya kila aina ya uovu. Yaani taqwa maana yake ni kinga ya Mwenyezi Mungu.

Istilahi taqwa ina maana ya kuwa chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu kwa kutafuta kinga Kwake, kuepuka kile kilichoharamishwa na kufuata kwa utii kile kilichoamrishwa; ina maana ya kuogopa adhabu na mateso ya Mola Mtukufu na kutafuta kivuli cha Rehema Zake. Kwa sababu hiyo, kuua matamanio ya nafsi na kustawisha kipawa cha roho ndilo jambo muhimu. Kwa maneno mengine, taqwa ni kurejea katika utukufu wa maamrisho ya Qur'an na Sunna, na hii ndiyo njia ya furaha ya milele katika maisha ya kifamilia, kibiashara na kijamii-kwa kifupi, furaha huwepo katika kila kipengele cha maisha yetu.

Taqwa yaweza kuelezewa kama ni utekelezaji wa maamrisho ya Uislamu kwa shauku, heshima na ridhaa. Ina maana ya kuzingatia barabara maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu na kuepuka dhambi kwa gharama zote.

Taqwa ni kitendo cha kutaadabu nafsi kwa undani wa (aya hii) "Amefaulu yule aliyeitakasa nafsi yake." (A'la, 87:14).

Ni pale tutakapokuwa tumefanya hivi ndipo nyoyo zetu zitakapokuwa zimepata utulivu katika imani, ibada, na katika matendo anayoyaridhia Mwenyezi Mungu.

Taqwa ni muungano wa kiroho baina ya muumini na Mwenyezi Mungu; Taqwa ni kiashirio cha sifa bora kama huruma, ukarimu, usamehevu, upole na utengenefu ndani ya moyo, na pia taqwa ni hali ya kutafuta radhi za Allah kwa kila tendo, kila jambo na kila kitu.

Taqwa ni toba ya kweli ya yule mtu anayedumu katika hali ya kutafuta maghfira kwa ulimi na moyo.

Taqwa ni hali ya moyo kujaa mapenzi kwa Mwenyezi Mungu na hofu juu ya Adhabu Yake.

Taqwa ni hali ya kuukinga moyo na fikra mbaya.

Kuitia elimu vitendoni ndiko kunakomzidishia mtu hikima, na imani ya kweli katika kuuchunga moyo ndiyo taqwa yenyewe. Ndiyo sababu maana sahihi ya imani haishii katika maneno matupu au akili tupu ya kujenga hoja, bali imani ni tamko la moyoni la kukubali kuitumia elimu katika njia yetu ya maisha kwa namna ya kupata radhi za Allah. Jambo hili huwezekana kwa ile nafsi tu iliyojaa taqwa ya hali ya juu kabisa.

Kwa namna fulani, taqwa ni kinga ya moyo dhidi ya chochote kile kinachomtenga mtu mbali na MwenyeziMungu huku moyo huo ukifurahia kuwa karibu na kitu chochote kitakachoukurubisha zaidi kwa Mwenyezi Mungu.

Taqwa maana yake ni kufuata Amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (saw) kwa mapenzi na mahaba makubwa, kuutazama ulimwengu mzima kwa huruma na upole wa Muumba, na kuchukizwa na chochote kinachokwenda

kinyume na jambo hili, kujiweka mbali na jambo au tendo lolote linaloweza kuharibu nafsi.

Taqwa ni kiashirio cha chuki dhidi ya chochote kile kinachoitenga nafsi mbali na Mwenyezi Mungu. Kwa hali hiyo, taqwa ni kuyafisha matamanio ya nafsi na kustawisha vipawa vya roho ambavyo Mwenyezi Mungu amemjaalia mwanadamu.

Taqwa ni moyo ambao umefanya jihadi ya kujitakasa; na wale waliofaulu kupata utakaso huo, moyo wao huwa hazina ya khulka njema

**MOYO WA MUUNGWANA**

Mtume Muhammad (saw) alionesha mfano wa tabia za marafiki wa Mwenyezi Mungu. Wakati mwingine alikuwa akiwauliza Maswahaba maswali ambayo yaliifanya jamaa nzima itege sikio zaidi, na alikuwa akiuliza maswali ili apate kutoa ufafanuzi wa mambo kadha wa kadhaa. Katika moja ya fursa hizi, Mtume (saw) aliwauliza Maswahaba, “Je yupo mtu yeyote miongoni mwenu anayeweza kuwa kama Abu Damdam?” Maswahaba wakaulizas “Abu Damdam ndio nani?” Mtume (saw) akajibu: “huyu alikuwa ni mtu wa kabila moja lililokuwapo kabla ya zama zenu, yeye alikuwa akisema: ‘nimewasamehe wale wote walionitukana na kuniteta.” (Abu Dawud, Adab 36:4887).

Huu ni mfano wa taqwa: moyo wenye maungwana ya hali ya juu!

Hallâj-i Mansûr yeye alinyoosha mikono yake juu kuwaombea dua wale waliokuwa wakimpiga na mawe, akiomba ulinzi wa Mwenyezi Mungu. Aliomba hivi: “Ewe Mwenyezi

Mungu! Hawa watu hawajui: Kabla ya kunighufiria mimi, wasamehe wale wanaonipiga mawe!”

Taqwa ni imani ya hali ya juu iliyowapelekea Maswahaba kuwa karibu na Mtume (saw). Anas (ra) kasimulia kuwa mtu mmoja alimuuliza Mtume Muhammad: “Ni nani ahali zake Muhammad?” Mtume akajibu, “Kila Muttaqi (mwenye taqwa) ni mmoja wa ahali zangu.” Hivyo basi, twaona kuwa kila muumini anayefikia utengenefu kwa taqwa huheshimika kwa kiwango cha kuhesabiwa kama mwanandugu wa familia ya Mtume.”

**TAQWA HUJUMUISHA HATUA TATU**

1- Kuepuka yaliyokatazwa

2- Kushikamana na maamrisho. Hii ni shurti ya kutimizwa na waumini wote na ndiyo ngazi ya msingi ya taqwa.

3- Kujawa na hisia za kujihudhurisha kwa Mwenyezi Mungu wakati wote. Hiki ndicho kiwango cha juu kabisa, na ndicho kipimo halisi cha elimu na taqwa.

Katika Qur’an, Mwenyezi Mungu kabainisha kuwa Yeye yu “karibu zaidi kuliko mshipa wa shingo.” (Qaf, 50:16), na muda wote Yeye yu pamoja nanyi popote mlipo.” (Hadyd, 57:4).

Muungano huu una maana kuwa mtu hupambika kwa sifa za Mwenyezi Mungu na huishi kwa kujitambua kuwa Mwenyezi Mungu yupo naye muda wote. Nafsi inayopambika kwa vazi la taqwa (guo la uchaMungu) ndiyo inayopata mwongozo wa kuielekeza upande wa haki na kuiwaidhi kukataa batili na munkari; wenye nafsi hii ndio watakaotambua thamani na maana halisi ya vitu vya kidunia.

Qur'an ni sanaa andishi ya Mwenyezi Mungu ambayo humsaidia mwanadamu kutatua kila tatizo analokabiliana nalo. Ni kupitia Qur'an na Sunna ndipo tunapoweza kupata amani na furaha.

Qur'an ni upambanuzi wa maisha ya mtu. Asili ya mwanadamu inapatikana ndani ya Qur'an na Qur'an ndiyo umbile la walimwengu wote; ulimwengu ndiyo anuani ya Qur'an.

Mtu anapofikia kilele cha taqwa, utambuzi wake wa Qur'an na ufahamu wake wa ulimwengu huzama ndani kabisa na huambatana na hikima na imani ya ghaibu juu ya ulimwengu. Kwa uimbaji mwororo wa ndege aimbaye usiku, kwa mneso wa matumba ya ua la waridi, kwa mtiririko maridhawa wa mito itoayo sauti ya utulivu, twaweza kupata ibra ya mapambo na neema za ulimwengu. Hapo ndipo tunapoanza kufahamu undani wa imani ya Yûnus Imre pale alipozungumza na ua la njano kuhusiana na maana ya ibra zake mwenyewe.

Taqwa ya kweli ndiyo ishara ya kumfikia Mwenyezi Mungu. Ibn Atậ'llậl al-Iskandari yeye alisema kuwa muumini mwenye moyo thabiti husema hivi baada ya kupata taqwa: Ewe Mwenyezi Mungu, wamepoteza nini wale waliokufikia Wewe; na wamekuta nini wale waliokutupa Wewe?" Kanuni ambayo waumini wote wanapaswa kuifuata ni hii:

## KUWENI NA TAQWA KATIKA KILA JAMBO

Maisha ni ya kupita, yanapita na raha na shida zake. Wakati mwingine ni ya dhiki na ufukara; na wakati mwingine ni ya utajiri na faraja; na wakati mwingine, ni machungu na majonzi, na kuna wakati maisha yanajaa amani na furaha. Wakati wa raha na shida, mwenendo wa muumini wa kweli

uwe ule ulioelezwa na Mtume: "Muwe na taqwa katika dhiki na faraja." Mtume (saw) alituasa tusiwe waumini katika mazingira fulani tu bali tumche Mungu katika mambo yote.

Rumi kasema: "Usibabaishwe na raha wala tabu kwa sababu roho yako ndiyo makazi ya raha ilihali tabu na furaha ni wageni wa kupita tu."

Katika nyakati za shida, ni muhimu kuwa na subira na kuomba msaada wa Allah bila mtu kupoteza dira lake. Katika nyakati za utajiri na neema, mtu anapaswa kuongeza shukurani kwa neema hizo za Allah bila ya kufanya isirafu wala kujivuna mbele ya wengine. Tusiharibu maisha yetu kwa kufuata matamanio ya nafsi zetu katika vipindi vya neema na raha.

Tunapokabiliana na shida, tumshukuru na kumtukuza MwenyeziMungu bila manung'uniko! Kumsabihi na kumuhimidi Mwenyezi Mungu kwa mafanikio na neema zitokazo kwake na kujinyenyekesha kwa Mwenyezi Mungu kwa moyo wa subira nyakati za shida ni wajibu kwa kila mtu. Tunapaswa kusema: "Hili ndilo ambalo Mwenyezi Mungu kaliona ni kheri kwangu." Hiki ndicho kipimo cha taqwa.

Baada ya kushinda vita kubwa ya Maka, Mtume (saw) aliwakumbusha Maswahaba kuwa hii ilikuwa ni rehema ya Mwenyezi Mungu na akawafunza kumsifu na kumtukuza MwenyeziMungu. Aliwanasihi kuwa "maisha ya kweli ni maisha ya Peponi." Licha ya taabu na mitihani waliyokabiliana nayo kabla ya kushinda vita ya Khandaki, Mtume (saw) aliwanasihi Maswahaba kuwa na subira akisema: "Maisha halisi ni maisha ya Peponi." Katika aya nyingi, Qur'an inatueleza namna ya kuishi maisha ya taqwa ambayo ndiyo yanayotakiwa kwetu na Mwenyezi Mungu: Kwa hakika, Qur'an ndiyo;

## MWONGOZO KWA WALE WENYE TAQWA

Bila shaka, Qur'an ni neema kubwa, ndiyo chanzo cha utajiri wa nafsi na mafanikio ya kiroho kwa wanadamu.

"(Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema amefundisha Qur'an, amemuumba binadamu, akamfundisha kunena." (Rahman, 55:1-4).

Kwa aya hii, Mwenyezi Mungu anasema dini na Qur'an ndio msingi wa maisha ya mwanadamu, kwamba viwili hivyo ndiyo sababu ya kuumbwa kwa ulimwengu. Mwenyezi Mungu anabainisha maudhui ya Qur'an tukufu kwa kusema: "Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni mwongozo kwa wamchao Mwenyezi Mungu." (Baqara, 2:2).

Hatuna budi kuyachunguza matendo yetu kwa kuzingatia aya hii na tuyatathmini maisha yetu kwa kujiuliza je tutaulizwa nini kaburini na je maisha yetu ya Milele yatakuwaje Akhera? Je hali yetu itakuwaje Siku ya Hesabu pale ulimwengu utakapokuwa umefutiliwa mbali nasi tutakapokuwa katika siku kubwa kabisa? Je tuishi vipi katika dunia hii ili kunusurika na wakati huo wa kutisha, na kusalimika katika Siku hiyo ya Hukumu?

Tunapata mafundisho gani kwa maneno haya ya Umar bin Abdulaziz, "jiandae na maisha ya Akhera kulingana na vile unavyoyatarajia yawe?"

Qur'an ndiyo mwongozo wa kutuongoza katika maswali yote haya yanayohusiana na safari ya milele; ni mwongozo wa kuyaendea maswali haya na majibu yake, ndiyo mwongozo wa taqwa. Njia za kutokea moyoni ambazo huelekea kwenye maudhui ya ndani ya Qur'an huanza kupanuka kulingana na kiwango cha taqwa kilichofikiwa na Muumini.

Hisia za mtu hutakaswa na kulainishwa na huepukana kabisa na matamanio ya nafsi, na kwa kufanya hivyo, ndipo mtu anapomkurubia zaidi Mwenyezi Mungu. Hapo MwenyeziMungu huwa macho ambayo kwayo watu walio karibu naye huonea, huwa masikio ambayo kwayo husikilia na ndio huwa nyoyo za utakaso."

Kwa kufanya hivyo, tafakuri huzama ndani ambapo mtu hutambua lugha ya maua yachanuayo, lugha ya ndege waimbao na lugha ya miti itoayo matunda. Kwa kutafakari rehema, hadhi na hisani hii katika maisha ya kiroho, ndipo watu wanaporuzukiwa nafsi za kheri.

Hao ndio muttaqiina waliosifiwa katika Qur'an. Wanafanana na mito itiririshayo maji ambayo yamewapatia uhai zaidi ya maelfu kwa maelfu ya viumbe hai,kuanzia binadamu, mimea, waridi hadi maua ya kila aina. Kituo chao cha mwisho ni kile cha kukutana tena na Mola wao katika maisha ya milele. Kwa hiyo, taqwa, kimsingi, ndiyo hatua ya kwanza ya ya kumkurubia Mwenyezi Mungu. Qur'an inawafahamisha watu wa taqwa kwamba wanapaswa:

## KUTAFUTA NJIA YA KUMFIKIA YEYE

Katika Qur'an Mwenyezi Mungu anasema: "Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kumfikia. Na piganeni kwa ajili ya dini Yake ili mpate kufaulu." (Maida, 5:35).

Ni zipi njia sahihi za kumkurubia Mwenyezi Mungu? Utwaharifu wa mtu, utakaso wa nafsi, utii, ibada, mapenzi ya dhati moyoni juu ya Mwenyezi Mungu, Kuzidisha mapenzi na hofu mbele ya Mamlaka Tukufu ya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu anatutaka tuzitafiti njia hizi. Katubainishia kuwa lengo halisi tunalopaswa kulipa umuhimu na kulizingatia katika maisha yetu ni Akhera. Ulimwengu uliopo hivi sasa ni kijitone kiduchu mno cha maji baharini kulinganisha na ule wa milele.

Qur'an yatwambia kuwa Siku ya Hesabu tutaulizwa tuliishi vipi maisha yetu. Sisi tutajibu eti tuliishi kwa muda wa siku moja, au nusu siku. Tunatakiwa na Mwenyezi Mungu kujitahidi katika maisha haya kupata hata kijitone kiduchu kabisa cha taqwa cha kutuwezesha kupata Bahari hiyo ya Pepo. Lakini juhudi hiyo ni ya kiwango gani?

Kiwango cha taqwa kinachotakiwa kwetu ni kile cha kututosha kusimama mbele ya Utukufu wa Mwenyezi Mungu kwa heshima na staha fulani: yaani

**KWA KUMNYENYEKEA MWENYEZI MUNGU**

Mwenyezi Mungu anasema katika Qur'an: "Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha." (Aali Imran, 3:102). Hii inatutaka tutumie njia na jitihada zetu zote kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa imani, ibada na tabia".

Kwa vile ni muhali kwetu kujua kiwango halisi cha jitihada kinachohitajika katika kuonesha heshima mbele ya Utukufu wa Mwenyezi Mungu, basi hatuwezi kupuuzia hata amali ndogo kabisa. Kuhusiana na hili ipo amri ifuatayo: "Na msife hadi mmekuwa Waislamu."

Tunaweza tu kufikia ngazi na daraja fulani katika dunia kwa jitihada zisizo na ukomo, na ingawaje tunaweza kudumu na jitihada hizi katika maisha yetu, lakini bado jitihada hizo si

hakikisho la mwisho la maisha yetu ya kiroho. Qur'an inatufahamisha kuhusu wale walioangukia kwenye upotevu katika pumzi yao ya mwisho, hao ni watu kama Bal'am bin Bawra na Qarun.

Qarun, mtu wa zama za Nabii Musa, ndiye aliyekuwa mfasiri mashuhuri wa Taurat katika enzi zake. Mwenyezi Mungu akampa mali kama mtihani. Baada ya hapo akawa mtu wa kutegemea mali hiyo kiasi ambacho alijivuna kwa kumwambia Musa hivi: "Kila kitu ni changu mwenyewe. Nimevichuma mimi mwenyewe." Ndipo Mwenyezi Mungu alipomwangamiza na kumdidimiza yeye na mali yake aliyoipenda na kuitegemea kwa kiasi hicho kikubwa. Mali yeke haikumfaa chochote ndani ya giza totoro la ardhi.

Bal'am bin Bawra, baada ya kufikia daraja mbalimbali za imani katika enzi za uhai wake, mwishoni kabisa akafa katika hali ya upotofu na upotevu kwa sababu ya kufuata matashi na tamaa yake na kuifuja ilimu yake. Kama alivyoangamizwa Qarun kwa kufuja mali yake, Bal'am naye aliangamizwa kwa kufuja ilimu yake.

Mwenyezi Mungu anatuamrisha tujikinge kwa taqwa pale anaposema: "Na umuabudu Mola wako mpaka ikufikie hiyo yakini," (Hijr, 15:99), kama vilevile anavyotuwaidhi kuwa kuukinga moyo kwa taqwa ndilo jambo muhimu katika maisha haya.

Ewe Mwenyezi Mungu! Tujaalie uwezo tuachane na kila kitu na tusimame mbele yako kwa nguvu halisi ya taqwa! Tuwezeshe kudumu katika ibada hadi mwisho wa pumzi yetu! Na utupe hadhi ya kusimama mbele Yako kama umma wa Waislamu!

Âmîn!

# Kheri ya Moyo Uliotakasika: *Ikhlas na Taqwa-II*

## SIRI YA NUSRA (WOKOVU)

Baadhi ya aya za Qur'an Tukufu huanza na kiapo ili kuvuta mazingatio ya hadhira juu ya muradi wa maudhui. Mara nyingine, kiapo hutambulisha jambo linalohusiana na maisha ya waja wa Mwenyezi Mungu. Kuna nyakati na nyakati ambapo idadi ya viapo huongezeka kulingana na uzito mkubwa wa mada husika. Mathalani, Mwenyezi Mungu Mtukufu anaanza sura ya 91, al-Shams, kwa viapo saba. Kila kimoja kinatambulisha mojawapo ya maumbile ya ulimwengu-jua, mwezi, mabadiliko ya mchana na usiku, mbingu, utii na nafsi-hadi, mwishoni, ambapo Mwenyezi Mungu anazungumzia (mafanikio ya) jihadi ya ndani ya nafsi na (hasara ya) uovu wa nafsi hiyo, akimbainishia mwanadamu njia ya kupatia nusra, 'Naapa kwa nafsi na Aliyeitengeneza, kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake, bila shaka amefaulu aliyeitakasa (nafsi yake), na bila shaka amejihasiri aliyeiviza (nafsi yake). (Shams, 91:7-10).

Qur'an inabainisha kuwa, kwa upande mmoja, nafsi ya binadamu yaweza kuendeshwa na matamanio ya kimwili na kushawishika kutenda dhambi, na kwa upande mwingine,

nafsi hiyo hiyo inayo nafasi ya taqwa. Uelekeo wa kwanza wa nafsi hiyo ni ule wa kutamani kutopea kwenye machafu ya ulimwengu, wakati ule wa pili ni wa roho yenye kutaka kutanua mbawa zake na kuogelea mawinguni.

Rumi anasema yafuatayo kuhusiana na jambo hili:

"Ewe msafiri wa haki! Kama unastahabu kuujua ukweli, basi si Firauni wala Musa aliyekufa, wote wako hai ndani ya mwili wako, wamejibanza ndani ya uhai wako. Wanaendelea na mapambano yao ndani ya moyo wako. Hivyo basi, yakubidi uwatafute mahasimu hawa wawili ndani ya nafsi yako."

Hivyo basi, twaweza kuona kuwa taqwa ndiyo jambo muhimu katika kuomba ulinzi dhidi ya adui huyu wa mwanadamu ambaye yuko mapambanoni naye katika kila dakika ya uhai wake. Dua ya Mtume Muhammad (saw) ya kuomba MwenyeziMungu amjaalie taqwa ni kigezo kwa waumini: "Ewe Mwenyezi Mungu Ijaalie roho yangu taqwa na Ijaalie nafsi yangu utakaso. Wewe ndiwe Mmiliki wa roho yangu na ndiye mlezi wa nafsi yangu." (Muslim, Dhikr, 73). Muumini atafaulu katika mapambano dhidi ya nafsi yake kama atadumu na jihadi katika kila kipengele cha maisha yake; lazima aishi ndani ya mipaka ya taqwa katika kila jambo la maisha yake, kuanzia imani hadi ibada yake. Kwa kuzingatia hili, moja ya shurti za dini ni:

## TAQWA KATIKA IMANI

Imani isiponawiri kwa taqwa, basi upungufu mwingi wa kimaumbile katika tabia za mtu hubakia palepale; jambo hili ndilo linalopelekea imani kudhoofika na hatimaye huifanya ikose maana kabisa; kinachofuata baada ya hapo ni mtu ku-

tumbukia kwenye ujahili na ushirikina. Ndiyo sababu taqwa ni jambo muhimu mno.

Taqwa ndani ya imani huanza kwa kuipa kinga tauhiid. Mtume Muhammad (saw) amesema: "yeyote anayetamka lâ ilâha illallâh katika dakika za mwisho za uhai wake hapa duniani, huyo ataingia Peponi." (Hâkim, Mustadrak, 1:503). Lakini je, hii tauhiid hukingwa vipi? Hatua ya kwanza ya kufanikisha jambo hilo huanza kwa ufahamu sahihi juu ya upweke wa Mwenyezi Mungu.

Kwa kule kusema *lâ ilâha,* masanamu yote huondoshwa moyoni ili zidhihirike sifa Njema. Sifa hizi Njema huwa hazishamiri pale ambapo moyo umechafuka kwa sababu ya kuzongwa na mawazo ya hovyo, katika mawazo haya ya hovyo, ndimo ulimo mchafukoge wa fikra za kipuuzi au ndimo inamopita njia ya kibubusa. Moyo lazima utakaswe na fikra mbaya, khulka mbaya, na tabia mbaya. Mwenyezi Mungu anasema: Je, umemuona yule aliyefanya matamanio yake kuwa mungu wake?" (Furqân, 25:43) Akiashiria hatari za kufuata hisia mbaya na matamanio mabaya ya moyo."

Kutakasika kwa nafsi na kutengenea kwa nafsi ni mambo muhimu kwani moyo ndiyo makazi ya imani. Mizizi na shina la imani humea pale imani inapostawishwa. Ndiyo sababu kuimarisha imani ndani ya nafsi ni jambo muhimu. Ndiyo kusema kuwa kumuamini Mwenyezi Mungu ni jukumu la moyo na si lile la akili.

Mambo ya ghaibu na mambo yaliyofichakana ya ulimwengu huambatana na nguvu ya moyo na si nguvu ya akili ya mtu. Mambo ya ghaibu hufahamika kwa njia ya moyo. Anasema Rûmî: "Ni muhali kukifikia kina kisichokoma cha dini, nafsi iliyoerevuka tu ndiyo inayoweza kukitamani kina hicho."

Nafsi iliyo na ufahamu huru wa mambo yenye yakini isiyo na ukomo wa mipaka, yenyewe tu huwa ni ulimwengu kamili wa mambo ya dhahiri na mambo ya ghaibu. Kutokana na ile asili ya nafsi ya kutetereka na kubadilikabadilika kirahisi, kazi ngumu katika dini ni ile ya kudumisha imani baada ya mtu kumuamini Mwenyezi Mungu na kuamini mambo mengine ya ghaibu. Mtume (saw) amesema: "Moyo uko kama unyoya ambao hupeperushwa na upepo katika jangwa." (Ibn Mâjah, Muqaddimah, 10; Ahmad, IV: 408, 419).

Mabadiliko ndani ya moyo ndiyo yanayoweza kusababisha imani kuyumba. Kuukinga moyo kwa taqwâ ndiyo njia pekee ya kulinda imani. Hivyo, tuwe hadhiri;

## USIRIDHIE WALA KUUELEKEA UOVU

Hakuna maridhiano ya Imani; mtu hapaswi kuwaelekea makafiri au watu waovu.. Moja ya sifa za moyo ni kwamba huwa inashawishika na wale inaojenga mapenzi kwao. Hivyo, Mwenyezi Mungu anasema, "Wala msiwategemee wale wanaodhulumu (nafsi zao kwa maasi); usije ukakuguseni Moto." (Hûd, 11:113), akiashiria kuwa muumini lazima aikinge nafsi yake dhidi ya mapenzi kwa madhalimu na waasi.

Kamwe tusighafilike kuwa Mwenyezi Mungu hataki nyoyo zetu zitiwe shirki ya chochote kile zaidi Yake. Kumpwekesha Mwenyezi Mungu maana yake ni kwamba katu tusiruhusu kitu chochote kuingia moyoni; tusikaribishe matamanio ya nafsi wala tusiwaonee huruma madhalimu na waovu.

Tumuombe Mwenyezi Mungu atukinge hasa hasa dhidi ya maadui wa imani na dhidi ya kujenga hisia za mapenzi kwa wale wanaopinga Uislamu kwani jambo hili linaweza kuitia

hasara nafsi. Imâm Ghazali anasema: "Kujinasibu na mawazo ya makafiri baadae hugeuka na kujenga uhusiano wa moyoni; mapenzi haya yatakuwa maangamizi kwa mtu."

Tahadhari hizi za Mtume Muhammad (saw) zina umuhimu mkubwa kabisa: "Pale mwovu anaposifiwa, Mwenyezi Mungu hughadhibika na ardhi hutetemeka." (Bayhaqi, Shu'ab, IV:230).

"Msimwite mnafiki mfalme, kwani hilo litamfanya kafiri huyo awe kinara wenu na hapo mtakaribisha Ghadhabu za Muumba wenu kwa kufanya hivyo." (Abû Dâwud, Adab, 83; Ahmad, V:346).

"Yeyote anayejifananisha na umma, basi naye huhesabiwa kama ni mmoja wao." (Abu Dawud, *Libas*, 4:4031).

Taqwa ndani ya imani pamoja na kinga ya moyo vina umuhimu huo kwamba Mtume aliwaamrisha Maswahaba zake kufunga tarehe 10 ya Muharram ikiwa ni pamoja na siku moja kabla yake, na siku moja baada yake ili kutofautisha mila ya Waislamu na mila ya Wayahudi (katika dini ya Uyahudi, ipo funga moja tu ya tarehe 10 ya Muharram).

Hivyo basi, Mtume Muhammad alijenga msingi wa aina yake wa mila ya Kiislamu na akatupatia mwongozo. Kuitimiza mila hii ni sharti la kiimani. Kwa sababu hiyo, hatuna budi kuchukua tahadhari kubwa katika kuzigubika nyoyo zetu kwa taqwa. Kutenganisha moyo na mwili ni sawa na kuukata kwa kisu kimakosa mshipa mkubwa wa damu, lazima mtu afe kwa kupoteza damu. Kujenga uhusiano wa moyo na watu wasiofaa bila kuwachuja kutaupelekea moyo kupoteza utakaso wa nafsi na kusababisha umezwe gizani.

Moyo ndio kiungo kinachosadikiwa kujitegemea chenyewe mwilini kwani wenyewe huendelea kudunda hata pale

ubongo, "kituo cha maamrisho", unapokuwa umekufa. Ikiwa hali ndiyo hiyo basi, tahadhari ya kuepuka matendo yasiyofaa ina umuhimu mkubwa mno, kwani Mwenyezi Mungu anasema katika Sura ya tisa ya Qur'an, Tawba, 'Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu...' (9:119). Ili kuzikinga nafsi zetu dhidi ya vishawishi vinavyoweza kutukengeusha tumepewa amri hii na Mwenyezi Mungu:

**KUWENI PAMOJA NA WAKWELI**

Ni sehemu ya umbile letu la kibinadamu kwamba huwa tunaathiriwa na watu tunaozoeana nao. Hivyo, ni muhimu kujihadhari na mambo yasiyofaa na kuzingatia yale yanayofaa katika mazingira tunayoishi na tujihadhari na wale tunaoishi nao. Mtu asipokuwa hadhiri na athari anazokabiliwa nazo, basi hiyo yaweza kumsababishia upungufu wa taqwa na hata kumpeleka kwenye maangamizi.

Taqwa hukingwa kwa kuulinda moyo dhidi ya shari ya watu na kwa kuijaza nafsi kheri. Kuna mkondo unaotiririka baina ya moyo wa mtu mmoja na mwingine. Mpepeso tu wa jicho la mtu mmoja waweza kusomba kiwango cha athari kinachotosha kuleta mabadiliko ndani ya nafsi zetu. Hata hivyo, athari ya moyo nayo huwa kubwa zaidi kulinganisha na hiyo.

Wanadamu wanaweza kuwa watiifu kwa wakweli na madhalimu; hivyo, kinga ya ukweli hupatikana kwa kuwa pamoja na wakweli na watiifu, na sio kuwa pamoja na wenye nyoyo ngumu na wenye kudhulumu.

Daruweshi mmoja aliwahi kumuomba Bâyezidi Bistâmî: "Ninasihi kuhusu tendo litakalonikurubisha zaidi kwa Mwe-

nyezi Mungu." Nasaha zikawa hizi: "Wapende Marafiki wa Mwenyezi Mungu! Wapende ili nao wakupende. Jitahidi kuingia ndani ya nyoyo zao; Mwenyezi Mungu huangalia mara mia tatu na sitini kwa siku ndani ya nafsi za watu walioangaziwa nuru, na akiliona jina lako ndani ya moyo wa mmoja wao, basi Atakughufiria."

Sifa maalum waliyokuwa nayo Maswahaba ni kwamba walidumu moja kwa moja katika kundi la Mtume na hivyo kupata tija ya imani na neema iliyotokana na Unabii. Neno Maswahaba lina maana ya wale waliokuwa katika kundi la Mtume, ndio kusema mujitamaa huu wa kimwili na kiroho wa Mtume ndio uliowatukuza Maswahaba. Mujitamaa huu umekuwa ukiendelea tangia wakati wa Mtume hadi leo.

Sâdî Shirâzî, akifafanua faida za kuwa pamoja na wakweli, alisema: "Yule mbwa wa Vijana wa Pangoni (Ashâb-i-kahf) alipewa heshima kubwa kwa sababu alikuwa pamoja na watu watiifu; mbwa huyo katajwa katika Qur'an na katika vitabu vya historia."

Rûmî naye alitoa kauli hiyo hiyo: "Mbwa yule alihiyari kuwa pamoja na Maswahaba wa Pangoni. Kwa kule kufurahia kwake kuwa pamoja nao, naye atabaki palepale mbele ya mlango hadi Siku ya Hesabu. Yeye hatakuwa na chakula badala yake atakunywa maji ya huruma na atakula chakula cha rehema."

Nafsi inapojitenga na watu wa kweli na badala yake kujijumuisha na watu waovu na kughafilika na Mwenyezi Mungu ndio basi huangamia. Hakuna mtu atakayeongoka katika makundi haya mabaya au jamii hizi mbaya hata akiwa na akili, ufahamu au utambuzi gani. Mathalani, Lut, japo alikuwa nabii, lakini alikumbana na shari ya watu wake na hivyo, hakukuwa

na mtu katika jamii yake aliyeweza kuelewa wahyi alioupokea; matokeo yake Lut akauliza kwa mshangao: "...Je, miongoni mwenu hakuna muongofu (hata mmoja)?" (Hud, 11:78).

Katika aya nyingine (Tahrim, 66:10), Qur'an inawataja wake wa Nuhu na Lut, ambao walihiyari kuwa pamoja na watu waovu badala ya kuwa pamoja na manabii hao (waume zao), na hivyo kupigwa laana ya kuingia Motoni. Hata wake wa Manabii hawatanusurika na adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa maovu yao. Hivyo, kwa upande mmoja, mbwa, kwa sababu ya kuwa pamoja na watu wema, kapewa nafasi muhimu ndani ya Qur'an, lakini kwa upande mwingine, wake hao wawili waasi wa Manabii wameangamizwa milele.

Kwa kulitilia hili maanani hivi leo ambapo imani iliyopo ni ndogo mno, ilihali ndio wakati ambapo tunaukaribia mwisho wa dunia, taqwa ndiyo ya kuchukua uzito mkubwa zaidi, kwani kuishika imani ya kweli hivi sasa ni:

## SAWA NA KUSHIKA KAA LA MOTO

Katika Hadith moja, Mtume Muhammad (saw) amesema: "Ole wao Waarabu, kwani shari kubwa inawanyemelea. Itakuwa kama mapingapinga ya usiku. Mtu atasimama asubuhi akiwa muumini lakini ukiingia usiku anakuwa kafiri. Watu watauza dini yao kwa bei ndogo. Mtu atakayeshikilia dini wakati huo atakuwa kama yule anayeshika kaa la moto." (Ahmad, II:390; Muslim, Iman, 186; Tirmidhi, Fitan, 30:2196).

Katika aya nyingi za Qur'an, matendo mema hutajwa sanjari na imani kwani taa ya imani ni ibada na vitendo; ni kwa sababu hii ndio maana daraja la pili muhimu la taqwa ni

## TAQWA KATIKA IBADA HASAHASA SWALA

Tutaikurubia zaidi Taqwa kadri tunavyozidi kuchunga utekelezaji wa faradhi za ibada zilizoamrishwa kwetu kwa mnasaba wa maisha yetu na kama sehemu ya utumishi wetu kwa Mwenyezi Mungu. Ni ibada iliyosalimika na utovu wa hushui na inayofanyika kwa nia ya kupata radhi za Allah ndiyo tu itakayotengemaa. Kwa mfano, twavijua vipengele sahihi vya Swala; lakini undani halisi wa hekima yake ni kumuhudhurisha mtu mbele ya Mwenyezi Mungu. Huu ni mkutano tuliopangiwa ili tukidhi mahitaji yetu ya kiroho na kimwili. Je hii swala ina ukaribu gani na kile kilichoelezwa na kinachotakiwa kwetu na Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema? Kama ilivyobainishwa katika Qur'an: "Bila shaka Swala humzuilia (mwenye kuswali) mambo machafu na maovu." (Ankabût, 29:45).

Je Swala zetu ziko hivi? Aya ifuatayo ilishushwa ndani ya Qur'an kuutaka moyo wa muumini uwe katika hali ya kujirudisha kwa Mwenyezi Mungu pale mtu anaposujudu: "... sujudu na uwe karibu (na Mungu wako)." (Alaq, 96:19). Je sijda yetu iwe ya kiwango gani cha utimilifu?

Hali za familia zetu, biashara zetu na majukumu yetu ya kiofisi vyote viwe taswira za namna tunavyoswali. Kama kweli tunaswali kwa usahihi basi maisha yetu ya kifamilia nayo yatakuwa ya taqwa, maisha yetu ya kibiashara yatakuwa ya uaminifu na utimizaji wa majukumu yetu ya kiofisi utakuwa bora zaidi.

Mwenyezi Mungu kabainisha ifuatavyo kuhusiana na wale wasiopata manufaa ya swala zao na ambao nyoyo zao zimejaa dhambi: "Basi adhabu kali itawathubutikia wenye kuswali." (Mâ'ûn, 107:4). Qur'an inasisitiza uangalifu katika kuhifadhi Swala, kuidumisha na kuiswali kwa unyenyekevu.

Kama vilevile unavyohitajika usafi wa mwili na utakaso wa roho kabla ya Swala, ndivyo unyenyekevu wa moyo nao unavyohitajika-moyo lazima uguswe na uwe hadhiri kuwa tunasimama mbele ya Mwenyezi Mungu. Mtume Muhammad (saw) amesema, Mwenyezi Mungu Mtukufu anaupenda kila moyo uliojaa unyenyekevu (kwa Allah), huzuni (kwa sababu ya kuhisi kuwa haujatimiza wajibu kama ilivyoamrishwa) na huruma, Yeye anawapenda wale wanaowafundisha watu mema na kuwalingania wamtii Mwenyezi Mungu." (Daylami, I:158).

Mtume (saw) aliwahi kumuona mtu mmoja aliyekuwa akishikashika ndevu zake wakati akiswali; Mtume akatahayari: "Tazameni na zingatieni, laiti moyo wa mtu huyu ungelikuwa na unyenyekevu wa kweli basi viungo vyake navyo vingenyenyekea." ('Alî al-Muttaqî, VIII, 197:22530).

Mfano mwingine wa taqwa katika Ibada ni

**TAQWA KATIKA FUNGA**

Funga ni zoezi la kujinyima, au upunguzaji wa matumizi ya vitu na mambo ya halali, hii ni kujizuia na chakula na matendo ya halali wakati wa mchana (tangu alfajiri hadi jioni). Ukamilifu na taqwa katika funga vyalazimu kutanua masharti ya funga katika maisha yetu ya kila siku, tuishi kwa kuepuka ulafi, kuepuka isirafu na kuepuka vya haramu na vyenye kutia shaka.

Funga hutuonesha jinsi tunavyoishi kwa kutegemea kipande cha mkate na glasi ya maji: hii ni njia nyingine ambayo kwayo Mwenyezi Mungu anatukumbusha namna tunavyoishi kwa kumtegemea Yeye. Wale wanaoifikia taqwa katika ibada pia hupata hisia hizo hizo za kiroho zitokanazo na funga.

Watu hawa huweza kutafakari thamani ya neema walizoneemeshwa na Mwenyezi Mungu na hujawa na mapenzi kwa wale ambao, kwa kiasi fulani, wamekosa neema hizo. Hisia za huruma kwa wenye njaa huongezeka katika kipindi cha swaumu, na, kwa hali hiyo, huruma hiyo hubainika katika swadaka.

## TAQWA KATIKA UTOAJI WA SADAKA

Wakati wa kutoa swadaka yatupasa kutambua kuwa hiyo mali tunayotoa mwenyewe hasa ni nani. Waumini wanapaswa kufikia kiwango ambacho wautazame ulimwengu kwa macho ya Muumba, yaani, wautazame kwa huruma na ukarimu. Hivi ndivyo tunavyoita kuwa ni kuifikia taqwa katika kutoa Swadaka.

Wakomunisti husema: “mali ni mali ya jamii” huku Mabepari wakisema, “mali ni mali ya mtu.” Uislamu unasema: “mali ni amana tu waliyokabidhiwa wanadamu, kila kitu ni riziki ya muda, Mwenyewe hasa ni Mwenyezi Mungu”. Hivyo, ndani ya mipaka hii, yule aliyekabidhiwa amana hana haki ya kuifanyia ubakhili wala isirafu.

“Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anapokea toba ya waja Wake na kuzipokea sadaka, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kukubali toba sana (na) Mwenye rehema?” (Tawba, 9:104).

Aya hii daima ibakie vichwani mwetu kama kipimo cha taqwa yetu katika utoaji wa msaada na swadaka; kipimo hiki ni kutoa bila kutarajia au kutafuta sifa wala hadhi na bila hisia za kujifaharisha moyoni. Badala yake mtu aseme: “Lillah, Ewe Mola wangu, hiki kinachotolewa, kinatolewa kwa ajili

Yako". Hivi ndivyo vipimo sahihi vya swadaqa. Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kakibainisha kipimo cha taqwa na ukarimu katika swadaka kama ifuatavyo: "Msiharibu sadaka zenu kwa masumbulizi wala udhia." (Baqarah, 2:264). Hii inabainisha wazi taqwa ambayo mtu anapaswa kuwa nayo pale anapotoa swadaka.

Abû l-Layth Samarkandî kanena hivi: "Ukweli kuhusu utoaji wa swadaka ni kwamba mtu anayetoa ndiye anayepaswa kutoa shukurani kwa yule anayepokea, kwani, kwa kupokea huko, mpokeaji anakuwa amemuepushia mtoaji aina nyingi za matakwa ya nafsi na pia anakuwa amemuepushia shari na mabalaa; juu ya yote hayo, mtoaji anakuwa amepata radhi za Allah."

Baba yangu mpendwa, Musa Efendi, alikuwa na hisia kali sana juu ya ukarimu aliowanyia watu wakati akitoa kitu: alistahabu kuwaepushia wapokeaji wa swadaka ile adha au fedheha ambayo wangeihisi, na hivyo, alikuwa akiandika juu ya bahasha hivi: 'Mpendwa fulani bin fulani, tunakushukuru kwa kupokea hii'. Shukurani hii ya dhati kutoka moyoni mwake kwenda kwa mpokeaji ilikuwa na sababu kwamba kile kilichokuwa kinatolewa kiliambatana na imani kuwa yeye mtoaji, Musa Efendi, ndiye angenufaika zaidi kwa kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie kiwango hiki cha taqwa pale tutoapo swadaka. Amin!

Kama tulivyofafanua huko nyuma, taqwa ni kama kiungo cha ghaibu ambacho kinapaswa kuwepo kwenye msingi wa kila faradhi ya dini; kwa ajili hiyo, jambo la kwanza tunalopaswa kulitafuta katika ibada zetu ni taqwa. Hija ni faradhi nyingine ya kimwili ya dini kama ilivyo zaka, ambayo hutekelezwa katika mazingira yanayofanana.

'Amali' anayoihitaji Haj ni ile ambayo, kadri anavyokabiliwa na magumu wakati akiwa katika ihram, ndivyo moyo wake unavyozidi kutakasika ili upate rehema za Mwenyezi Mungu.

**TAQWA WAKATI WA HIJJA**

Hija ni wajibu uliofaradhishwa, kifedha na kimwili ambapo mbali ya vipengele hivyo vya kifedha na kimwili vya Hija, hija ya mtu mwenye taqwa hujumuisha uhudhuriaji wa kiroho mahali pale patakatifu na hujumuisha tija ya kiroho. Kuyazingatia masiku yanayopitishwa huku ukivaa nguo inayofanana na sanda na kuzidumisha hisia hizi za kiroho ni sehemu ya Hija.

Hatuna budi kuutafakari utii wa Ibrahim pale tunapompiga mawe Shetani. Wakati wa Hija pasiwe na maneno yasiyohitajika, pasiwe na kitendo cha dhambi na pasiwe na ugomvi! Lazima tuepuke mazingira na matendo ya kutuweka mbali na Mwenyezi Mungu; kujiepusha na tabia ya ugomvi na mabishano na kudumu na mwenendo huu katika maisha yetu ya kila siku ndiyo matunda ya taqwa yatokanayo na ibada ya Hija.

Tunapokuwa Hija, ni haramu kuwinda au kuchuma jani la mti wenye uhai. Ni haramu hata kumsakiza mwindaji kwa kumuelekeza eneo muhimu la mawindo. Lengo hapa ni kutufunza kudumisha huruma, upole na hisia katika maisha yetu ya kila siku.

Hivyo basi faradhi za dini yetu, kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na swala, funga, kutoa zaka na kuhiji, lazima zifanywe kwa ikhilaswi na kwa utaratibu sahihi wenye taqwa, sio kwa msimu tu; sifa hizi lazima zikite mizizi ndani ya nyoyo zetu. Iwapo hatuwezi kulifikia hili, basi hii ina maana kuwa moyo

bado haujafikia kiwango cha taqwa. Waumini wazichambue nafsi zao ili wabaini vikwazo ambavyo vimewakwaza kulifikia jambo hili.

**VIKWAZO VITATU VYA TAQWA**

Cha kwanza katika vikwazo hivi ni kujifaharisha. Yaani, kujivuna. Hii ina maana kuwa tunavichukulia vipawa na vipaji vyetu kuwa ni vyetu wenyewe ingawaje, kwa kweli, ni vya kupewa na Mwenyezi Mungu. Kwa hali hiyo, na sisi tunakuwa kama Ibilisi, Firauni na Qarun ambao walihesabu kila kitu kuwa ni chao wenyewe. Hâjî Bayram-i Walî kasema kuwa majivuno ni sawa na jiwe lililofungwa kiunoni; ambapo huwezi kuogelea wala kuruka.

Kikwazo cha pili ni ubakhili; yaani kuwa mgumu wa kutoa (fedha), kukataa kutumia wasaa au nguvu kwa ajili ya majukumu na matendo ya kila siku ya dini. Yatupasa kuuzingatia ukweli kuwa "Pepo ipo kwa ajili ya Mukaramuna na Jahanamu kwa ajili ya wafanyao ubakhili. (Imam Ali).

Kikwazo cha tatu ni upumbavu. Mtu anayeitupa Akhera akistahabu upofu wa dunia, akihiari kuishi maisha ya mghafala kuliko ulimwengu wa milele, huyo ni mpumbavu.

Kuhusiana na yale mambo yanayoweza kuharibu taqwa, Mtume Muhammad (saw) amesema maneno haya: "Utafika wakati ambapo hakutakuwa na kitu cha kupendwa zaidi kama hivi vitatu: chumo la halali, udugu wa kweli na Sunna yangu." (Haythami, 1:172). Kuchuma mali ya halali (kujipatia fedha kihalali), kufaidi udugu wa kweli uliojengeka kwa ikhilaswi na kwa kuishi Kisunna ni mambo yanayowezekana kwa kufuata mwongozo wa kweli na kwa matendo mema. Ndiyo maana kipengele kingine cha taqwa ni

**TAQWA KATIKA MWENENDO**

Taqwa ya tabia na hisia huhitajika katika kila kipengele ili kuhakikisha hali ya kufurahi na kurithika kwa binafsi na kwa jamii. Mathalani, taqwa ndani ya huruma maana yake ni kutoa ulichonacho kuwapa wasionacho na mafakiri. Kwa maneno mengine, huruma maana yake ni kuhangaika kuwasaidia wasionacho katika jamii.

Huruma ndiyo sifa ya asili ya nafsi ya muumini katika dunia hii na ndiyo chanzo cha habari njema ya furaha ya milele Akhera. Kupata rehema za Mwenyezi Mungu ni neema kubwa itokayo kwa Mwenyezi Mungu, kwani inatokana na huruma. Wale wanaowahurumia wengine ndio wakarimu, ndio wenye huruma na ndio wenye kutambua wajibu wao kwa wengine.

Hivyo, tunapokuwa wazima wa afya, hatuna budi kuifikiria hali ya wenzetu wenye ulemavu, mayatima na wasionacho. Lazima tutambue kuwa wao ni dhamana tuliyopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu; Mwenyezi Mungu kawaleta watu hawa kama mtihani kwetu, kwani muumini ana dhamana kwa nduguye wa imani na ana dhamana kwa walimwengu. Huu ndio mkataba wa Uislamu.

Ndiyo sababu muumini lazima ajihehesabu nafsi yake muda wote na apime kiwango cha huruma alichonacho. Huruma ndiyo ladha tamu ya imani. Rahman, Mwingi wa Rehema, na Rahim, Mwenye kurehemu, ni majina mawili ya Mwenyezi Mungu yanayotajwa mara kwa mara ndani ya Qur'an. Hii inatubainishi kuwa Mwenyezi Mungu anawataka waumini watengenee kwa sifa ya huruma.

Akiongozwa na Hadith, Rûmî anapendekeza tija ya huruma kwa muumini:

"Wahurumieni wale waliofukarika zaidi yenu ili wale waliotajirika zaidi yenu nao waoneshe huruma kwenu." Mtume Muhammad (saw) amesema, "Naapa kwa Yule anayeshikilia roho yangu Mkononi Mwake, hamtaingia Peponi mpaka muamini, na hamtaamini mpaka mpendane. Maswahaba wakaitikia, "Ewe Mtume wa MwenyeziMungu, sisi ni wenye huruma," kwa kuzingatia huruma waliyoonesha kwa watoto wao na familia zao. Mtume akajibu, upendo ninaouzungumzia sio ule wa ndugu zenu tu; upendo huu unajumuisha ulimwengu mzima, naam ulimwengu mzima" (Hâkim, IV, 185:7310).

Imesimuliwa kuwa wakati Mtume alipokuwa njiani kuelekea Maka akiwa pamoja na jeshi la Waislamu, alikutana na mbwa kando ya barabara akiwanyonyesha watoto wake. Basi Mtume akalimrisha jeshi kukata upande mwingine wa barabara ili wasimkarahishe mbwa huyo na watoto wake. Mara nyingine, Mtume alikiona kiota cha wadudu chungu kimechomwa moto, akalalama: "Haimpasi yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu kuadhibu kwa moto!" (Abû Dâwud, Jihâd, 112). Huruma inapojikita kwenye nafsi, mtu hufikia:

**HALI YA KUJALI ZAIDI WENGINE (îthaar)**

Hatua inayofuata ya huruma ni utu kwa watu. Hii ina maana ya kuwafikiria wengine kabla ya kujifikiria wewe mwenyewe. Hiki ndicho kiwango cha juu kabisa cha huruma. Hii ni hali ambayo Mwenyezi Mungu anapenda kuiona kwa waumini. Ndani ya Qur'an, Mwenyezi Mungu amewasifu Ansâr ambao walionesha kuwapendelea zaidi Muhajirun kuliko nafsi zao.

"Na (pia wapewe) wale waliofanya maskani yao hapa (Madina) na wakautakasa Uislamu (wao barabara) kabla ya (kuja) hao (Muhajiri huko Madina) na wakawapenda hao waliohamia kwao, wala hawapati, hawaoni dhiki nyoyoni mwao kwa hayo waliyopewa, na wanawapendelea kuliko nafsi zao ingawa wenyewe wana hali ndogo. Na waepushwao na ubakhili wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kwelikweli." (59:9).

Hii ndiyo sifa kubwa waliyopewa wale waliopata taqwa kwa huruma na moyo wa kuwajali wengine. Moja ya sifa muhimu za marafiki wa Mtume ni kwamba huwajali wengine kabla ya nafsi zao ambapo nafsi zao hukingwa na mitego ya shetani kwa sababu ya taqwâ ya kweli.

Ubaydullâh Ahrâr kasimulia: "Mtu mmoja alikuja na kusema, 'Nina njaa, je mnaweza kunilisha?' Na mimi pia nilikuwa na njaa, lakini sikuwa na pesa wala njia yoyote ya kujipatia chakula. Nikampeleka masikini huyo kwa mpishi na kumwambia, 'Mimi sina pesa lakini kilemba nilichovaa ni twahara. Unaweza kukitumia kukaushia sahani, na fidia ya kitambaa hiki, mlishe chakula mtu huyu mwenye njaa. Mpishi huyo akampa bwana huyo sahani ya chakula, na japokuwa na mimi nilikuwa na njaa, nikakaa naye tu wakati yeye akila. Nikavua kitambaa na kumpa mpishi. Kwanza alikataa akisema kuwa hataki kitambaa hicho. Hapo nikamwambia: 'nilikupa ahadi, basi kichukue. Baada ya hapo, Mwenyezi Mungu akanineemesha utajiri. Nilikuwa na wafanyakazi elfu mbili shambani kwangu. Kisha nikachukua dhamana ya kuwatunza watu wawili ambao hawakuwa na hali nzuri. Walianza kujifukia udongo wenyewe kutokana na ukali wa maradhi waliyougua. Nikaleta maji kuwasafisha; baada ya muda mfupi, nikadhibiti maradhi hayo, lakini nikaendelea kuwahudumia."

Hebu ona kiwango kikubwa kilioje hicho cha moyo wa kujali wengine na huruma alichoonesha bwana huyo.

Hawa ndio watu wanaotimiza amri hii: “Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu.” (Baqara, 2: 195). Hawa ndio wabakiao katika njia ya taqwa kwa matendo yao ya kuwafanyia hisani viumbe wote wa Mwenyezi Mungu. Hawa ndio watu wa kuufikia utengenefu na ndio wa watu watakaoifikia hisani. Kwa hiyo, umuhimu wa taqwa katika matendo ni:

**TAQWA KATIKA IHSAAN (WEMA)**

Neno Ihsani hujitokeza kwa sura mbalimbali zaidi ya mara mia moja na tisini ndani ya Qur’an. Kwa kuzingatia moja ya maana ya maana zake za msingi, ili kuijua hisani, muumini lazima aoneshe hisani kwa kadri iwezekanavyo katika kila kipengele cha maisha, iwe katika moyo wake, mazingira yake, biashara yake au nyumbani kwake. Maana nyingine za Ihsan ni kuwa hadhiri kuwa kila kitendo kinaangaliwa na Mwenyezi Mungu; hivyo basi taqwa katika Ihsani na ukarimu ni kitu kinachohitajika katika kila hatua tunayopiga katika maisha.

Mwisho, hali ya muumini muda wote iwe ile ya uzuri, ubora na utengenefu. Hii hupatikana kwa njia ya imani na taqwa katika unyenyekevu, na hii ina maana kuwa muumini muda wote aulinganishe utii wake kwa Mwenyezi Mungu na utii wake kwa waumini. Mwenyezi Mungu anaielezea hali ya moyo wa muumini katika aya ifuatayo:

‘Hakika waumini wa kweli ni wale ambao anapotajwa Mwenyezi Mungu, nyoyo zao hujaa khofu; na wanaposomewa Aya zake huwazidishia imani, na wakamtegemea Mola wao tu basi.’ (Anfâl, 8:2).

**“Ewe Mwenyezi Mungu! Zitie nguvu imani zetu na vidhubutishe vitendo vyetu kwa taqwa na tujaalie kiwango cha taqwa cha kukuridhisha Wewe. Tujaalie tuwe miongoni mwa wale ambao nyoyo zao hutetemeka wanaposikia jina Lako, wale ambao imani zao huzidi kuongezeka wanaposoma kila aya ya Qur’an, na tujaalie tuwe miongoni mwa wale wanaokuabudu Wewe Peke Yako.**

**Âmîn!**

# Kheri ya Moyo Uliotakasika:
## *Ikhlâs na Taqwâ-III*

**TAQWA KATIKA KURIDHIA (RIDA)**

Mazingira na matukio hujitokeza katika sura nne: zile ambazo ni za kheri na zile za shari

1-Kuna watu ambao ni wema ndani ya nafsi zao na kwa Sura ya nje:

Mtu anayehangaika kujitafutia maisha kwa kazi ambayo inakubalika Kiislamu na anayetumia pesa zake kwa ajili ya mambo ya kheri, mara kwa mara akitoa swadaka, akifanya matendo ya hisani kwa wanadamu wenziwe, wanyama na mazingira, kwa mikono yake, kauli zake na tabia yake, na anayechunga vya haramu na vya halali na anayeepuka chochote chenye shaka huku moyo wake ukibaki umejaa ikhilaswi na taqwa, basi hiyo ni ishara ya wema ndani na nje ya nafsi yake.

2-Kuna Watu ambao ni Wabaya Ndani ya Nafsi na kwa Sura ya nje

Hii ni hali ya wale wanaoyaendea mambo ya kuchukiza na kudhalilisha katika dunia hii. Mambo yote yaliyoharamish-

wa huangukia katika kundi hili. Wakiamini kuwa msiba ndiyo furaha kwao, watu hawa huishi kwa kuzidanganya nafsi zao hapa duniani na hawatapata chochote ila huzuni ya Akhera.

3- Matendo ambayo ni Mema kwa Sura ya Nje lakini Mabaya kwa Sura ya ndani:

Kuna mambo fulani ambayo huonekana mema yanapotazamwa kwa sura ya nje, lakini yanapochunguzwa kwa upande wa ndani, hubainika kuwa mzizi wa wema wake huo ni uovu. Mathalani, mali inayoambatana na bughudha kwa dhiki waliyonayo wengine kwa sababu ya nafsi ya kujikweza.

Mali yaweza kuonekana kama neema, lakini ubakhili na isirafu katika mali hiyo ni maovu yanayozidisha dhambi na adhabu ya mtu papa hapa duniani na Akhera. Mifano mikuu ya hili ni Qârûn na Sâlebe ambao wote walikumbwa na maangamizi. Walizidanganya nafsi zao na wakaendelea kupuuzilia mbali maamrisho ya Mwenyezi Mungu ili wachume mali, wakidhani ndiyo ya kuwafaa. Huku wakikadhibisha mawaidha ya Manabii, wakaghafilika kwa uovu wa matendo yao. Matokeo yake, wote wawili wakaangamizwa katika msiba ulioangamiza maisha yao katika dunia hii na Akhera.

Aya ifuatayo ya Qur'an inaelezea hali ya watu hawa:

"Lakini mwanadamu, Mola wake anapomfanyia mtihani Akamtukuza na kumneemesha, basi husema: 'Mola wangu amenitukuza. Na anapomfanyia mtihani Akampunguzia riziki yake, husema: 'Mola wangu amenidhalilisha!" (Fajr, 89:15-16).

Kamwe tusighafilike kuwa utajiri na umasikini vyote vinatoka kwa Mwenyezi Mungu; lazima turidhike na chochote ambacho Mwenyezi Mungu anaona kinatufaa na tutimize majukumu yetu kwa kuzingatia masharti ya vile ambavyo tumeruzukiwa. Hapa ndipo inapoanzia swadaka ya kweli.

Tukighafilika na ukweli huu na kupuuza Amri ya Mwenyezi Mungu huku tukizidi kuendelea na mambo yaliyokatazwa, basi hali yetu itakuwa kama ilivyoelezwa katika Qur'an: "Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayejua (lakini) nyinyi hamjui." (Baqarah, 2:216). Muumini aliyeneemeka ni yule anayefahamu jambo hili na anayeishi kwa kuzingatia ufahamu huu katika kila kipengele cha maisha yake.

Sifa kubwa sana ya Mtume Muhammad (saw) ambaye alijaaliwa sifa bora kabisa miongoni mwa sifa za binadamu, ilikuwa ni ile ya kuwa 'kiumbe aliyetengenea zaidi.' Nabii Suleiman hakuukumbatia utajiri, aliugawa utajiri wake wa duniani kwa walimwengu, alisifiwa na Mwenyezi Mungu kama ni 'kiumbe aliyetengenea'. Yunus yeye alikumbwa na mitihani mingi, alinyimwa afya, watoto na mali kwa miaka mingi; akiishi maisha ya shukurani na subira, aliukubali mtihani wake, na kwa hali hiyo, Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehama alimsifu kuwa alikuwa 'mja aliyetengenea' na akampa neema zisizokoma.

4-Mambo ambayo, kwa sura ya nje ni mabaya lakini ni mazuri kwa sura ya ndani

Mtu huwa mgonjwa ambapo kuzorota kwa afya yake japo kwaweza kuonekana kama jambo baya, lakini kwaweza kuwa jambo la kheri kwake kwani kutokana na ugonjwa huo, mtu huyo huweza kuutambua udhaifu alionao, na hivyo, kumkimbilia Mwenyezi Mungu na kumuomba msaada muda wote kutokana na tatizo hilo. Kwa hali hiyo, wema hudhihiri.

Abdullah ibn Mas'ud (ra) alisema: "Nilikwenda kumuona Mtume wa Mwenyezi Mungu ambaye alikuwa anasumbuliwa na homa. Nikamwambia, 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu,

inaonekana homa uliyonayo ni kali.' Mtume akajibu, 'Naam, ninasumbuliwa na maumivu ya watu wawili." Nikamwambia, 'Labda hivyo hivyo utapata rehema maradufu.' Mtume akajibu, 'Hakuna msiba unaomfika mwanadamu bila Mwenyezi Mungu kuufidia kwa dhambi zake, hata ule wa kuchomwa na mwiba.'" (Bukhari, Marda, 3,13,16).

Muumini wa kweli hana budi kuyapima matukio ya dunia hii ya mtihani kwa vigezo hivyo vinne vilivyoainishwa hapo juu na muda wote achunge sifa mbaya za moyo wake. Katika kila jambo, waumini wanapaswa kuitambua hadhi na daraja yao ya kuishi kwa kuomba toba, kumuhimidi na kumsabihi Mwenyezi Mungu.

Kila muumini mwenye ikhilasi hana budi kufanya jitihada za kufidia dhana zinazochukua nafasi kichwani mwake, hisia za moyo wake na hata pumzi anayovuta kwani kumridhisha Mwenyezi Mungu ndilo tunda bora kabisa la kustahabu. Kinachomfurahisha zaidi Mwenyezi Mungu ni pale muumini anapoyatupilia mbali matashi ya nafsi yake na kumtii Mwenyezi Mungu.

Sasa je tunawezaje kutambua wema na uovu ilihali vyote viwili haviwezi kudhihirika, tunawezaje kuvitambua ili kufikia aina hii ya moyo wa kuridhika. Swali hili lina jawabu moja tu

## KHERI IKO KWA MWENYEZI MUNGU TU

Katika kitabu, *Âmâk-i-Hayal*, kitabu cha hekima ya Usufi, kilichoandikwa na Ahmet Hilmi Efendi wa Filibe, kuna wahusika wakuu wawili; mmoja ni Aynali Baba, ambaye ni mtu mwerevu mwenye maneno ya hekima yanayoandamana na upigaji wa zumari (Ney). Muhusika mwingine ni Raji ambaye

ni mtu anayetafuta ukweli. Mara nyingi, watu hawa hukutana ambapo Aynali Baba hupiga Zumari, huwa wanajadili mambo fulani kuhusu ulimwengu na lengo la maisha.

Katika moja ya mikutano hiyo, wakati Raji alipokuwa akimsikiliza Aynali Baba anavyopiga zumari akashikwa na usingizi mzito. Akajiona yupo katika hadhara kubwa ya watu kuanzia manabii hadi wanafalsafa, watu wakubwa hadi watu wa kawaida. Mtu mmoja akasimama kuzungumza kwa niaba ya walimwengu. Huku akitokwa na machozi, akawauliza wanafikra hao wakubwa wa ulimwengu njia ya kuifikia furaha ya kweli: “Hebu niambieni, tafadhali oneni huruma; mimi nayachukia maisha yangu lakini nashindwa kuachana nayo. Tafadhali hebu niambieni raha ni kitu gani.”

Baadhi ya watu wakajibu. Confucias yeye akasema, “raha ni kupika wali hadi upikike barabara.” Plato yeye akasema: “raha ni kuufikiria utukufu mara kwa mara.” Aristotle akasema, “raha ni mantiki! Hiyo ndiyo raha hasa”Zoroastra akasema, “raha ni ile hali ya kutoachwa peke yako gizani.” Brahma akasema, “Nini raha? raha ni kinyume cha vile adhaniavyo kila mtu.” Budha akainuka kwa hamaki: “Enyi walimwengu! raha ni moja ya majina mazuri ya kitu kisichokuwepo, Nirvana (hali ya amani na utulivu aipatayo mtu kwa kuachana na matashi ya nafsi). Enyi walimwengu, dumuni katika hali hiyo (Nirvana).Watu waliosikia hivyo wakachanganyikiwa na kusema, “Basi hamjazifaa nafsi zenu; kumbe mmeishi maisha yenu bila raha na hakuna hata dalili ya raha katika kile mnachokihubiri!”

Hapo ndipo rafiki mmoja wa Mwenyezi Mungu aliposimama na kusema: “Kwa werevu, raha ni kuutazama uzuri wa Mwenyezi Mungu, ilihali kwa wajinga, raha ni ulafi na

ukware!" Kwa hakika, huyu ndiye aliyeibainisha raha kama walivyofundisha manabii.

Mwishowe, Kinara wa hadhara hiyo, Fahari wa Ulimwengu (saw) akasimama na kusema, Enyi watu! Raha ni kuyakubali maisha vile yalivyo, kuupokea mzigo na kukubali shida, na kufanya kila jitihada ya kupata hali bora; kwa maneno mengine, raha ni kupata moyo wa utakaso (moyo mweupe)." Baada ya kupata jawabu walilokuwa wakilitafuta, watu wakasimama na kuimba, "Ewe mbora wa walimwengu! Nabii Mbora wa Manabii! Ni wewe pekee ndiye unayeweza kuelewa na kugundua tiba ya walimwengu!"

Rumi, Mudiri mkubwa, alikuwa mwingi wa kusoma maisha ya watu: yeye alifahamu fika kuwa kheri ilitoka kwa Mwenyezi Mungu tu. Yeye alisema, "Hadi ukubali au uridhike kwa kile ambacho Mwenyezi Mungu kakiteremsha; popote unapokimbilia kutafuta nusura, fahamu kuwa utakabiliana na msiba; bila shaka, msiba utakuja na kukufika huko huko. Hakuna pembe yoyote ya ulimwengu iliyosalimika na mitego ya uovu. Hakuna cha kumtosha mtu wala cha kumuweka salama isipokuwa kuishi ndani ya amani ya kiroho; hivyo, mtafute Mwenyezi Mungu ndani ya roho yako na jikinge Kwake. Hakuna mahali ndani ya jela hii ya dunia ambapo hapatozwi malipo ya ulinzi na hakuna mahali ambapo watu hawapigiki huku na kule."

"Naapa kwa Jina la Mwenyezi Mungu kuwa ukitafuta hifadhi ndani ya shimo la panya, utanaswa na paka; njia pekee ya kutokea nje ni ile ya kuwa muumini wa kweli na kumfikia Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye atakayekufariji na kukukinga dhidi ya nyoka na nnge. Na mwishowe Yeye ndiye atakayekuwa rafiki yako."

Wakati mmoja, jini, kwa umbile la nyoka, alimtokea AbdulQadir Jaylani, mudiri mkubwa wa kiroho. Jini huyo akaondoka akiwa rafiki yake. Huu ni mfano wa rehema inayoletwa na mapenzi na radhi za Mwenyezi Mungu.

Kwa hiyo, wajibu wa waumini walioomba kheri yenye kudumu milele katika maisha ni kuridhia yote wanayokabiliana nayo kwa taqwa, ila tu wasiridhie kufuru (ukafiri) wala kuiacha njia sahihi. Maisha yakiendeshwa kwa njia hii, basi kifo na maisha baada ya kifo yatakuwa na faida ambapo mtu atafaulu Siku ya Hesabu.

Sharti jingine la kufikia kiwango hiki cha tabia njema ni uombaji wa toba na maghfira. Mwenendo wa nafsi unaotakiwa na Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema ni

## TAQWA KATIKA KUOMBA MAGHFIRA (MSAMAHA) NA TOBA

Sharti la toba ni kwamba majuto ya mtu yawe ya kweli; kujumuisha taqwa katika toba ndiko kunakotoa hakikisho kuwa mtu karejea kwa Mwenyezi Mungu katika hali ya kujitakasa na kuepuka moja kwa moja kutenda dhambi. Undani wa taqwa katika toba ni kutimiza ahadi ya kutotenda tena dhambi kwa uthibitisho wa matendo mema.

Muumini anapoondosha mapazia yaliyofunika uoni wa moyo wake ndipo anapouona mzigo wa dhambi unaoielemea nafsi yake na hapo ndipo anapoamsha hisia za wema ndani ya moyo wake. Nafsi ya mtu huyo hujirudisha kwa Mwenyezi Mungu huku akitokwa na machozi ya majuto; hii ndiyo toba ya kweli ya kujitoa katika dhambi na ndiyo ishara ya majuto ya kweli. Hii ndiyo njia ya kurudi kwa Mwenyezi Mungu.

Hivyo basi, kutubia ni hali ya kuondosha, kwa hisia za majuto, vizuizi vilivyopo baina ya muumini na Mola wake; siri ya toba ni mtu kuwa na moyo wa kusamehe. Mtu anayesamehe ndiye anayestahiki kusamehewa; kipimo kingine cha taqwa katika kuomba maghfira ni kwamba mtu anapoomba kusamehewa, basi na yeye ajitazame anavyoweza kuwasamehe wengine, ambapo kwa kuwasamehe wengine mara kwa mara ndipo mtu anapopata haki ya kusamehewa.

Ushauri ufuatao wa Sayidina Ali kwa mtu aliyeteuliwa kuwa Gavana ni muhimu sana: "Usiwatazame watu kama mbwa mwitu anavyolitazama windo lake! Uwe na mapenzi na huruma kwao kutoka ndani ya moyo wako! Bila kuwabagua, wao ni ndugu zako wa imani au ni wanadamu wenzio; wanaweza kutenda makosa. Wasaidie wenye kuhitaji na ukiomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu basi na wewe pia usamehe, wasamehe na wavumilie! Usighafilike, wala usipinzane na amri za Mwenyezi Mungu. Katu usiondoshe msamaha wako! Na wala usifurahie adhabu unazolazimika kuzitoa!"

Abu Darda (ra) ambaye ni mmoja wa Maswahaba wa Mtume, yeye alikuwa ni hakimu mjini Damascus pale aliposikia watu fulani wakimshutumu na kumzomea mtu mmoja aliyetenda dhambi. Abu Darda akawauliza, "Hivi ninyi mngefanya nini kama mgemuona mtu huyu katumbukia kisimani?" Wakajibu, "tungemtupia kamba na kujaribu kumuokoa." Hapo Abu Darda (ra) akasema, "mbona basi hamjaribu kumsaidia mtu huyu aliyetumbukia kwenye kisima cha dhambi?" Watu hao wakashangazwa sana kiasi cha kumuuliza, "Je wewe hukukasirishwa na mtenda dhambi huyu?" Abu Darda akatoa jibu la hekima sana, "Mimi nadharau dhambi zake, sio utu wake."

Kuna hekima kubwa katika utashi wa Abu Darda (ra) wa kutaka kupandikiza fundisho hili ndani ya nafsi za waumini. Hikima hii ina nuru ya maamrisho na radhi zaMwenyezi Mungu, ndiyo inayoakisi tabia ya Mtume katika nafsi za jamii. Njia pekee ya kupata raha ya milele katika ulimwengu huu wa muda ni kumuiga Mtume na kusambaza harufu ya manukato ya msamaha na mapenzi kutoka ndani ya moyo. Tunapokumbana na mikasa ya maudhi, yatupasa kuzigeuza nyoyo zetu kuwa makazi ya hekima yaliyojaa rehema za Mwenyezi Mungu na harufu nzuri ya Pepo, inayoambatana na msamaha, urafiki, huruma, uvumilivu na unyenyekevu.

Sifa nzuri ya taqwa ndiyo inayomtia mtu hamasa ya kuwafikiria wengine. Tabia ya mwanadamu inayopendwa mno na Mwenyezi Mungu ni ile ya kuhangaika kuwasaidia na kuwanusuru wengine. Hasahasa ni kwa

**KUAMRISHA MEMA NA KUKATAZA MABAYA**

Kuamrishana mema na kukatazana mabaya ndizo sifa kuu za muumini. Wajibu wa watu wamchao Mwenyezi Mungu ni kufanya jambo hili kwa vitendo na kwa ulimi na kunasihiana kutenda mema na kukatazana mabaya kwa upole. Iwapo Da'wa ya kulingania watu katika Uislamu na Ucha-Mungu vitaachwa, basi jamii itakuwa hatarini kukumbwa na maangamizi.

Zainabu bint Jahsh kasimulia kuwa yeye alimuuliza Mtume wa MwenyeziMungu, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, wakiwemo waumini miongoni mwetu, je tutaangamizwa?" Mtume (saw) akajibu, "Iwapo madhambi na maasi yatakithiri, basi ndiyo hivyo." (Bukhari, Anbiya' 7). Kwa hiyo, njia pekee ya kujikinga na Adhabu ya Mwenyezi Mungu ni ku-

waamrisha wengine kutenda mema na kuwakataza mabaya; hili ni jukumu la kila muumini mwenye taqwa.

Wakati wa kutimiza jukumu hili au jukumu lolote linalohusiana na hilo, mtu lazima aongozwe na Qur'an na Sunna, na ashauriane na watu wenye kujua katika kila hatua. Sayidina Ali alimpa gavana nasaha hizi: "Usiwapokee ndani ya Kamati ya shura wale wanaokutia hofu ya umasikini, au wanaojaribu kukuzuia kutenda mema; usiwapokee watu woga-woga wanaojaribu kukuchochea uzidi kuwa na tamaa au wale ambao wamepofushwa kutokana na matamanio yao!"

"Muelekee Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kwa ufumbuzi wa matatizo usiyoweza kuyatatua! Rejea kwa Mwenyezi Mungu na Kitabu Chake na rejea kwa Mtume Muhammad na Sunna yake."

Iwapo tunatamani kuwa miongoni mwa "Umma bora", basi lazima tuwe na maisha mema na tuwanasihi wengine kuishi kwa wema, kujiepusha na mabaya na maovu na vilevile kuwakataza wengine. Tutambue majukumu yetu katika njia ya Mwenyezi Mungu; bila hisia hizi za uwajibikaji na mapenzi, mtu hawezi kufanikiwa katika kuwanasihi wengine juu ya wema na ubaya. Cha muhimu ni

## TAQWA KATIKA KAZI YA KUUTUMIKIA UISLAMU (KHIDMA)

Msingi wa mafundisho ya Uislamu ni kumuelekea Mwenyezi Mungu kwa mapenzi ya kweli na ikhilaswi. Bila shaka, njia pekee ya kufaulu kulifikia hili ni kupitia utumishi. Wale wanaofanya kazi ya kuutumikia Uislamu ndio wajenge nguvu kubwa katika mazingira yao ili kila kitu kihuishwe kupitia

kwao; Kwa kuleta mwamko wa elimu katika mazingira yao, ndivyo na wao wanavyozidi kujiongezea mwangaza. Utumishi wa dhati ni matokeo ya moyo thabiti. Mafanikio katika kazi ya utumishi yanahitaji elimu, hekima, ufanisi, utulivu wa akili na tabia ya kujituma na haiba ya kiwiliwili.

Moyo wa mtumishi uwe kama udongo wenye rutuba; wale wanaopata mavuno katika udongo huo nao huacha jivujivu (la mabiwi) nyuma yao; kwa kusafisha (shamba) na jivujivu hilo, udongo huweza kuotesha mimea mbalimbali ambayo itawanawirisha viumbe wote wapitao.

Kwa sababu hiyo, wale wasio na ujuzi au uzoefu wa kutosha, ambao hawaupi umuhimu ustawi wa kiroho au wa maadili, wale watumishi ambao hawana ufahamu sahihi, wote hawa hawawezi kufanya kazi ya utumishi ya kuleta tija yoyote ile. Hatuwezi kutaraji matunda yoyote yaje kutokana na kazi ambayo imefanywa kwa umbambala na watu wa kukurupuka na wenye jazba ambao hawakupewa neema ya moyo wenye khulka njema.

Kwa hali hiyo, utumishi ambao umekosa utajiri wa nafsi ni sawa na ndoo ya maji inayomwagwa kwenye jangwa kame au mbegu iliyotupwa kwenye konde kame; itawadondokea panya wa shambani, itaishia patupu; mbegu za utumishi ambazo hupandwa na moyo ndizo zitakazogeuka miti ya kutoa matunda siku za usoni.

Wajibu mkubwa kabisa kwa wanadamu, ndani ya vigezo hivyo, ni ule wa kuwalingania kupata maisha (bora) ya milele. Njia pekee ya kuyafikia maisha hayo ni ile ya kuongozwa na mafundisho na mwongozo wa Qur'an na kufuata njia ya muumini wa kweli.

Dua ifuatayo ya Mtume (saw) iwemo katika nyoyo na Swala za wale wanaodumu katika kutimiza majukumu yao kama wanadamu: "Ewe Mwenyezi Mungu! Najikinga kwako na unyonge, uzembe, woga na kila aina ya udhaifu." Dua hii ya Mtume (saw) inatilia mkazo ulazima wa wepesi, umakini na uchangamfu.

Kwa kuzingatia hilo, wale wanaowalingania wengine lazima waoneshe upole ambapo kila jambo lifanyike kwa tahadhari kubwa. Kuwafahamu wale tunaowalingania ni wajibu tena ni wajibu mkubwa sawa na kazi yenyewe ili kuhakikisha kuwa kazi hii wanapewa wale wanaostahili zaidi. Wakati mwingine kumlingania mtu mmoja mwenye tabia njema kwaweza kuwa sawa na kulingania maelfu ya watu; kwani ukielekeza nguvu kwa mtu huyo mmoja mwerevu, nguvu hiyo haitapotea bure.

Jambo jingine muhimu la kulitilia maanani wakati wa kuwalingania wengine ni kuishi kwa hisia za shukurani. Sheikh Sâdi amesema, Msabihi Mwenyezi Mungu kwa kukuwezesha kufanikiwa katika kutenda mema, hii ni kwa sababu Yeye Mwenyezi Mungu ndiye aliyekufanyia wewe hisani na ndiye aliyekushushia rehema Zake. Watumwa wasimtarajie Sultan awashukuru wao kwa utumishi wao kwake, kinyume chake, wao ndio wamshukuru Yeye kwa kuwaajiri."

Tunapaswa kutambua kuwa undani wa hisani hiyo umo katika wajibu wetu kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (saw) kwani mtu mchaMungu anajua kuwa ameifikia taqwa kwa rehema za Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Vivyo hivyo, ni wajibu wa mtu kutimiza wajibu kwa wengine. Moja ya hisia nzito zaidi ndani ya moyo iwe ni

**TAQWA KATIKA UAMINIFU**

Maana ya msingi ya uaminifu ni kutomsahau wala kumtelekeza rafiki; mahusiano yote ya urafiki hudumu kwa msingi wa uaminifu. Pale hisia za kuaminiana zinapofifia, basi na urafiki nao hufifia, na uaminifu unapokufa, urafiki nao hukoma. Yawezekana kusema kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu aliishi maisha yake yote kama kigezo bora kabisa cha uaminifu.

Aliaminika kwa mama aliyemnyonyesha ambaye ndiye aliyemlea, aliaminika kwa wahabeshi ambao waliwapa hifadhi Waislamu waliohamia huko, aliaminika kwa Hadija ambaye alimuamini yeye wakati watu wengine walipomwita mwongo, na aliaminika kwa Maswahaba wake wote. Na hasa hasa aliaminika kwa Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema; hii ilikuwa ni aina tofauti kabisa ya uaminifu ambapo kuaminika huku kulidhihiri katika kila pumzi ya maisha aliyoishi Mtume.

Aisha (ra) kasimulia kuwa siku moja bi mkubwa mmoja alikuja kwa Mtume wakati Mtume akiwa pamoja naye. Mtume akamuomba bi mkubwa huyo ajitambulishe. Mwanamke huyo akasema: "Mimi ni Jassâmah wa Muzan" (Jassama maana yake ni 'mkubwa mno wa kimo') ." Kwa vile jina lake liliashiria sifa mbaya, Mtume akalibadili jina hilo akisema, "Hapana, kuanzia sasa na kuendelea wewe ni Hassanah wa Muzan (Hassanah maana yake ni urembo, uzuri)." Kisha Mtume akamuuliza alikuwa anaendeleaje tangu alipoonana naye mara ya mwisho kabisa. Bi mkubwa huyo akajibu: "Alhamdulillah, familia yangu na mimi mwenyewe hatujambo, naomba mama na baba yangu wajitoe muhanga kwa ajili yako!" Mwanamke huyo alipoondoka, Â'isha akamuuliza Mtume sababu ya kumpa heshima kubwa mwanamke huyo. Mtume wa Mwenyezi Mungu

akajibu: “Alikuwa akitutembelea mara nyingi wakati Khadija alipokuwa hai, na kuaminiana ni sehemu ya imani.” (Hakim, 1, 62:40). Wale waliotakasika kutokana na tabia njema ya Mtume na wao wakawa vielelezo vya uaminifu.

Cha kusikitisha ni kwamba uaminifu wenye shani hiyo sasa umekuwa zilipendwa; si kitu kilichomo tena katika nyoyo kwa sura yake halisi. Uaminifu umebaki kuwa neno tu la kupambia makamusi ya leo. Hapana shaka, hii ni kwa sababu ya kuporomoka kwa uchaMungu. “Kwa kila avunjae ahadi yake, kutakuwa na bendera (ya kumtambulisha) siku ya Hesabu, na itanadiwa kuwa bendera hiyo ni alama ya ahadi iliyotolewa na mtu huyo.” (Bukhari, Jizya, 22; Adab, 99 Hiyal, 99; Muslim, Jihad, 11-17)

Hapana budi isisitizwe kuwa wajibu wetu wa kwanza na wa msingi kabisa wa uaminifu ni kwa Mwenyezi Mungu na kisha kwa Mtume Wake Mtukufu (saw) ambaye ndiye sababu ya kuumbwa kwetu, ndiye furaha yetu ya milele na ndiye njia yetu ya imani. Hivyo basi, uaminifu lazima kwanza uelekezwe kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ambao wametufundisha na kutuongoza katika njia sahihi, kisha uelekezwe kwa mama zetu na baba zetu ambao lazima tuwahudumie wanapokuwa hai. Kuwa na adabu na kuwaheshimu wazazi wetu ni deni kubwa la uaminifu libwebalo na kijana au binti.

Uaminifu kwa wazee wetu, kwa wafu na kwa walio hai, uaminifu kwa taifa na kwa jamii nzima pia ni sifa ya tabia njema. Kwa hiyo, kila muumini aikinge taqwa yake, asisalimu amri kwa machafu ya zama hizi, na katu asiache kufanya jitihada za kulipa deni la uaminifu; vinginevyo mapenzi hupoteza thamani yake halisi na vivyo hivyo, urafiki na utumishi wake navyo hupoteza thamani yake halisi. Ni jukumu la mwanadamu kuilinda taqwa ndani ya uaminifu. Hata hivyo, lazima tutambue kuwa sharti la taqwa katika uaminifu ni

## TAQWA KATIKA MAPENZI NA MAHABA

Hatuwezi kufaulu kupata chochote bila ya mapenzi na mahaba ndani ya nyoyo zetu; Hata yale matendo madogo madogo kabisa huhitaji msukumo wa mapenzi. Vivyo hivyo, siri ya kuumbwa kwetu, siri ya maisha yetu, ni mahaba. Mahaba haya lazima yajengeke ndani ya mipaka ya taqwa kwani ni muhimu kuyatia nguvu mahaba kwa maadili sahihi. Wa kwanza kabisa katika wale tunaowapenda kikwelikweli lazima awe Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, na Mtume Wake (saw).

Mwenyezi Mungu kawajaalia waumini hisia za mapenzi ili wapendane kama ndugu wa Kiislamu. Kuchukia mambo mabaya ni jambo muhimu katika kuyalinda mahaba. Wema na ubaya hudhihiri kulingana na mapenzi . Kiwango cha mahaba ya mtu hulingana na kile akipendacho; Watu huwaonea hamu wale ambao wana mahaba nao; na huiga mfano wao; kwa hakika, mtu huathiriwa na wale anaowapenda.

Maswahaba wa Mtume walivuma kwa kila jambo na kila mahali kwa sababu ya mahaba yao kwa Mtume na kwa sababu ya baraka za Mtume (saw). Maswahaba ambao walikuwa karibu na Mtume pia walipata neema fulani ya maadili ya hali ya juu ya Mtume; Waislamu katika bonde la Hunayn walijenga ujasiri kutokana na Mtume, na Maswahaba wakapata unyenyekevu mkubwa kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya Mtume. Kwa kifupi, hadhi na mafanikio ya imani, ibada, maisha ya kifamilia, uaminifu na ukarimu wa Maswahaba vilikuwa ni taswira iliyoakisiwa kwa Mtume (saw). Maswahaba wakawa vile walivyokuwa kutokana na mahaba yao haya kwa Mtume.

Pale Mtume alipotawafu, maswahaba waligubikwa na

huzuni. Waumini ambao hawakuweza kuvumilia kupitisha siku bila kumuona Mtume ndio basi wasingeweza tena kumuona Mtume katika dunia hii. Ni jambo kuvutia kuwa katika kipindi hicho cha huzuni, Abdullah bin Zayd, ambaye alishindwa kuhimili hisia kuwa ndio basi asingeweza kumuona tena Mtume katika dunia hii, alinyanyua mikono yake juu kuomba dua kwa moyo wake safi: "Ewe MwenyeziMungu! Unyakue uoni wangu! Sitamani kuona kitu chochote katika dunia hii kama sitaweza kumuona Mtume mpendwa ambaye ninampenda mno!" Papo hapo akapoteza uoni wake.

Kuelekeza mahaba yetu kwa Mwenyezi Mungu kwahitaji kuipenda nuru ya Muhammad na wasifu wake mtukufu, kuwapenda Maswahaba, na kisha kuyatanua mapenzi hayo na kumpenda kila kiumbe wa Mwenyezi Mungu. Ishara moja kubwa ya maana ya mahaba kwa Mtume ni Sunna yake. Kwa mujibu wa usemi, "apendaye huabudu kila kitu kitokacho kwa apendwaye," kumfuata Mtume, kipenzi cha Mwenyezi Mungu, ni jambo muhimu. Kwa kiwango hicho hicho, tunaweza kufikia 'kigezo cha Mtume, kwa kutumia akili zetu, pia tunaweza kukifikia kwa mahaba.

Katu tusisahau kuwa mapenzi na mahaba tuliyonayo kwa mtu yeyote yule ulimwenguni badala ya Mwenyezi Mungu ni "mapenzi ya bandia", wakati mapenzi na mahaba ya dhati tuliyonayo kwa Mola wa walimwengu ndiyo 'Mapenzi ya kweli'.

Kwa maana hii, taqwa ni kuepuka chochote ambacho kitatutenga na Mwenyezi Mungu na Mtume; hii huweza kupatikana kwa kuwapenda wale ambao Mwenyezi Mungu na Mtume wanawapenda na kuwachukia wale ambao Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanawachukia.

**Ewe Mwenyezi Mungu! Tujaalie tuwapende wale Uwapendao na tuwachukie wale usiowaridhia! Usituzuilie utumishi, mahaba au utii kwa Mtume Wako Mtukufu! Tujaalie mapenzi ya kweli ndani ya mipaka ya taqwa! Na tuweke pamoja na Mtume Mtukufu duniani na Akhera!**

**Amin!**

# Neema ya Moyo Uliotakasika: *Ikhilas na Taqwa-IV*

**TAQWA KATIKA USAFI WA MOYO** *(IKHLAS)*

Ikhilaswi ni sharti muhimu kwa amali kukubaliwa na Mwenyezi Mungu. Ikhlaswi ni kwamba amali hizi zifanyike kwa ajili ya radhi za Mwenyezi Mungu pekee huku nafsini mwa mtu kukiwa hakuna kusudio jingine lolote lile. Ikhilaswi ina maana ya kuukinga moyo na kila aina ya maslahi ya kidunia ili kuwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu.

Ikhilaswi ndiyo kinga kubwa ya amali, bila ikhilaswi, nusura huwa ni muhali. Matendo bila ikhilaswi huishia patupu, hukosa thawabu. Kimsingi, Ikhilaswi ndiyo siri ya Mwenyezi Mungu, na kuipata siri hiyo kwa njia ya taqwa liwe lengo la kila muumini, kwani huu ndio msingi wa taqwa

Waumini wakiwa wakweli katika taqwa, kwamba, taqwa yao ina ikhilaswi, basi hii ina maana kuwa watu hao huwa na taqwa katika kila jambo. Lakini hii taqwa ni nini hasa? Miongoni mwa fafanuzi zilizopo, mojawapo ni kwamba pande zote mbili; upande wa roho wa na wa mwili wa mtu, zioane, na kwamba mtu awe na ikhilaswi na afanye mambo kwa uaminifu, akifanya jitahada kubwa za kujizuia na ubinafsi, unafiki, utovu wa ikhilaswi, na majivuno, vyote hivi huuwa ikhilaswi.

Sayidna Ali (ra), akizungumza na gavana yuleyule aliyetajwa huko nyuma, alitamka maneno mazito ya nasaha: "Usijisifu-sifu! Usimuheshimu yeyote anayekusifu mbele yako! Usiwakumbushie wengine kile ambacho umewafanyia. Usivikweze-kweze vitu ambavyo umefanikiwa kwavyo! Usivunje ahadi! Masimango huharibu amali njema, chumvi nyingi huharibu ukweli, na kushindwa kutimiza ahadi kwachochea ghadhabu za Mwenyezi Mungu na zile za jamii."

Tunapaswa kukumbuka kuwa Mtume (saw) alikataza majigambo, kwani yeye alitambua kuwa kila kitu ni neema kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Katika (vita ya) Khandaq, punde tu Maswahaba walipoanza kukata tamaa, katika kipindi chao kigumu mno, pale walipoulizana kama nusura ya Mwenyezi Mungu ingekuja, ndipo Muhammad (saw) alipowaambia, "Maisha halisi ni maisha ya Peponi." Halafu, katika kipindi hiki hiki mjini Maka, walipopata ushindi, Mtume Muhammad (saw) akasema, "Maisha halisi ni maisha ya Peponi," akidhihirisha kuwa yeye alimuamini na kumtii barabara Mwenyezi Mungu.

Mtume Muhammad (s.a.w) alijua kuwa ushindi na mafanikio, mali, uhai na watoto-kwa kifupi, kila kitu hutoka kwa Mwenyezi Mungu. Taqwa ndiyo ya msingi kwa sababu kotekote duniani na Akhera, msingi wa amani ni

## TAQWA KATIKA MALI, UHAI NA WATOTO

Hivi ndivyo vitu muhimu zaidi kwa mwanadamu, ni vitu ambavyo vinatutegemea zaidi sisi wenyewe na ndivyo vinavyotuathiri mno nafsi. Ni muhimu kuvitumia na kuvielekeza vitu hivu katika njia ya Mwenyezi Mungu, mtu atumie uhai na mali kwa moyo wa ukarimu, alee watoto kwa imani ili wawe

na manufaa kwa Uislamu, nchi na jamii, akiacha nyuma yake urithi wa imani kwa vizazi vijavyo.

Mwenyezi Mungu anaelezea kipimo cha mahaba katika moja ya aya za Qur'an: "Wala hamtakuwa wenye kuamini mpaka mtoe vile mvipendavyo."

Kwa hiyo, mali iliyo bora kabisa ni ile inayofika Akhera kabla mwenye mali hiyo hajafika huko na aina bora ya uhai ni ule unaotumiwa kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Wale wanaojua jinsi ya kutumia mali yao na uhai wao huwa kama nuru zing'arazo; wema wao na matendo yao mema huangaza hata katika sehemu za giza nene kabisa ambapo nuru ya mafanikio na ukarimu wao huenezwa kwa wenye shida, wasio nacho na walio taabani zaidi. Wajibu wa watoto ni kufanya jitihada za kupata radhi za wazazi wao, huku wazazi nao wakiwa na wajibu wa kupata radhi za Allah.

Ukweli wa mambo ni kwamba hata kama inaonekana kuwa mali na neema zetu katika maisha haya zinatoka kwa mama zetu, baba zetu au zinatokana na sisi wenyewe, lakini kwa uhalisi wake zote ni amana kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo basi, wajibu wetu ni kuwa na

**TAQWA KATIKA KUTUNZA AMANA**

Vyote vilivyomo baina ya Mbingu na ardhi vimekabidhiwa na Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kama amana kwa binadamu; kwamba ulimwengu mzima uliumbwa kwa ajili ya wanadamu na hivyo wote ni amana. Hivyo lazima tuoneshe mapenzi kwa viumbe vyote, ndiyo maana Mtume (saw) amesema, 'ukilazimika kumuua nyoka anayekushambulia basi muue kwa pigo moja ili asiteseke"?

Amana kubwa kabisa miongoni mwa amana hizo ni Qur'an na Sunna, hivyo, hatuna budi kukumbuka kauli iliyotolewa na Mtume Muhammad (saw) katika hotuba yake ya mwisho: "Enyi mlioamini, ninakuchieni vitu viwili vya thamani nyuma yangu, Qur'an na Sunna yangu. Mkivifuata hamtapotea kamwe." Hii ina maana kuwa kitu muhimu zaidi kilichokabidhiwa kama amana kwetu ni jukumu letu la kuubainisha Uislamu kwa kuzingatia Qur'an na Sunna katika imani yetu, matendo yetu, tabia zetu na mwenendo wetu.

Katika kila hali tunayokumbana nayo, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake hututarajia kuonesha moyo wa Kiislamu ambao ni moyo wa utulivu, heshima na ukomavu, ili watu wajifunze, "ni mtu mwema alioje Muislamu huyu!"

Qur'an haikutolewa kama amana kwa Muislamu ili ibakie kwenye kabati au isomwe kwenye mazishi au kwenye hafla nyinginezo. Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema ametuamrisha kusoma (iqra) Qur'an. Ili kufunuliwa mambo ya ghaibu na kupata hikima ya Qur'an, tumeamrishwa kuisoma Sunna ya Mtume. Aidha katika Qur'an kuna aya: "Na mwogopeni Mwenyezi Mungu, naye atakuelimisheni." (Baqara, 2:282).

Tukiishi ndani ya mipaka ya taqwa, basi kadri siku zinavyokwenda, mambo mengi zaidi ya ghaibu yatabainika. Ni wajibu wetu kulifahamu hili na kuzifahamu amana ambazo zimekadhiwa kwetu kwani wale wanaosubiri mwongozo kila mahali ulimwenguni nao ni amana kwetu; masikini ni amana kwetu, wakiwa ni amana kwetu, wanyonge na mayatima ni amana.

Utajiri umetolewa kwetu kama amana, watoto tumepewa kama amana; kwa kifupi kila kitu kimekabidhiwa kwetu kama amana. Inabainishwa katika Qur'an: "Na amekutiishi-

eni vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini-vyote vimetoka kwake; bila shaka katika haya zimo alama kwa watu wanaofikiri." (Al-Jathiyah, 45:13).

Ni aina ya huruma kuzifikisha amana hizi kwa wenyewe wanaostahiki. Kwa sababu hiyo, wale wanaozifikia sifa za juu, iwe kiimani, kifedha, kiakili au katika kuitumikia jamii – lazima watambue kuwa dhamana ya muda waliyonayo ni ya utimizaji wa amana. Wasizikumbatie dhamana zao kwani hawatabaki duniani milele.

Kwa upande mwingine, kama vile vile ambavyo ufujaji wa vitu umekatazwa katika Uislamu ndivyo hivyo hivyo ufujaji wa masurufu ya kiroho kama imani, ibada, elimu, wasaa na akili unavyokatazwa; kwa hakika, vitu hivi ndivyo vinavyoonekana kuwa hatari zaidi kwa mtu. Jambo muhimu ni kuzikinga amana zetu hizi kwa taqwa, ambapo jambo hili linahitaji hisia za uwajibikaji. Hivyo, kipengele kingine cha taqwa ni

**TAQWA KATIKA UWAJIBIKAJI**

Matendo yote, harakati zote na majukumu yote hustawishwa kwa msukumo wa uwajibikaji. Bila shaka, Mwenyezi Mungu amewajaalia wanadamu vipawa ambapo kila mmoja anawajibika kwa kadri ya uwezo aliopewa. Sote twatambua kuwa tunatakiwa kutoa moja ya arobaini (1/40) ya zaka, lakini ni vigumu kujua kima cha uwezo ambacho tumejaaliwa na Mwenyezi Mungu.

Ndio maana Mwenyezi Mungu hatutaki tupoteze nguvu zetu bure. Mwenyezi Mungu anasema: "Basi jitahidini kufanya mema" (Baqara, 2:148) na "Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife isipokuwa mmekwishakuwa Waislamu kamili." (Al-Imran,3:102).

Muumini lazima atambue jinsi anavyopaswa kuishi na afe katika mazingira gani. Lazima ajue namna ya kujielimisha ili kupata fadhila za imani. Kila pumzi tuvutayo hufuatia pumzi iliyotangulia na ndiyo pumzi ya kujiandaa na maisha yetu ya Akhera; hivyo basi, pumzi zitumike kufanyia vitendo vizuri. Ili kujihakikisha maisha ya furaha yaliyopambwa na amali njema , ni muhimu kuishi kwa heri na amani katika dunia hii; kuishi maisha ambayo hayakubaliki kwa Mwenyezi Mungu ni sawa na mazigazi (mangati) jangwani.

Kuna nyakati maalum zilizotengwa kwa faradhi za dini lakini imani na utumishi ni mambo ya wajibu katika nyakati zote maishani mwetu. Maisha yetu katika dunia hii ni ya muda maalum uliotolewa ili kujiandaa na Akhera ambapo ndipo tunapoweza kupata mapokezi ya Mwenyezi Mungu.

Njia ya kuungana na Mwenyezi Mungu ni njia nyembamba ya kuvuka iliyojaa mitihani na hatari; majukumu yake ni makubwa kiasi kwamba yalimbadili nywele Mtume zikawa nyeupe (mvi).

## NJIA PEKEE NI TAQWA

Kwa mujibu wa Hadith ya Abu Dharr (ra), siku moja Mtume alisema: "mimi naijua aya ya Qur'an ambayo, kama watu wangeizingatia, basi ingewatosha walimwengu wote." Maswahab a wakauliza, "Ni aya gani hiyo?" Mtume (saw) akaisoma: "Na anayemuogopa Mwenyezi Mungu, Yeye humtengenezea njia ya kuokoka." (Talaq, 65:2; Hadith Ibn Majah, Zuhd, 24).

'Njia ya kutokea' yaweza kufafanuliwa kama ni njia ya kutoka katika dhiki na kwenda kwenye faraja, kutoka ardhini

kwenda mbinguni, kutoka kwenye uduni kwenda kwenye thamani au ubora; ndiyo kusema basi, ubora katika Uislamu ni

## UBORA WA TAQWA

Mtume wa Mwenyezi Mungu alimuwaidhi Abu Dharr, akifafanua kuwa kigezo pekee cha kuthaminika na kukubalika mbele ya Mwenyezi Mungu ni taqwa. "Mtu mweupe hana ubora zaidi ya mtu mweusi isipokuwa kwa taqwa." (Ahmad, V, 158).

Mara nyingine, Mtume (saw) alisema, "Mimi ndiye mwenye taqwa zaidi miongoni mwenu." (Bukhari, Iman, 13; Muslim, Siyam, 74) Yeye aliishi ndani ya mipaka ya taqwa katika kila kipengele cha maisha. Hivyo, ni jambo muhimu kwetu kuwa waumini wenye taqwa na wanye kufuata Sunna ya Mtume Muhammad (saw). Kufuata Sunna na kuishi maisha yanayoendana nayo ni

## DALILI YA TAQWA

Nabii Isa aliielezea vizuri taqwa. Siku moja, mtu mmoja alikuja kwake na kumuuliza, "Mwalimu mwema, mtu huwezaje kuwa na taqwa mbele ya Mwenyezi Mungu?" Isa (Yesu) akajibu, "Hili mbona jepesi. Mpende Mwenyezi Mungu kwa moyo wako na fanya mambo mema kwa kadri ya uwezo wako. Onesha huruma na upole kwa wanadamu wote kana kwamba unaihurumia nafsi yako mwenyewe!" Kisha baadae akasema, "Watendee wengine kama ambavyo ungependa wengine wakutendee! Hapo kweli ndipo utakapokuwa mcha Mungu mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu." (Ahmad, Zuhd, uk.59).

Undani wa matendo na ibada ndio uzae kauli hii miongoni mwa Malaika kwamba;

**HII NDIYO TAQWA!**

Siku moja, 'Umar (ra) alimuuliza Ubayy bin Ka'b (ra) taqwa ni kitu gani. Ubayy akasema, "Ewe Umar umeshawahi kutembea kwenye njia yenye miba?" Umar akajibu, "ndio nimewahi." Ubayy akauliza, "ulifanyaje?" 'Umar akasema, "Nilikwida nguo zangu barabara na kutembea kwa tahadhari ya kukwepa miba." Ndipo Ubbay bin Ka'b aliposema, "basi hiyo ndiyo taqwa." (Ibn Kathir, Tafsir al-Qur'an al-Karim, 1:42).

Jua litakalotuangazia juu yetu iwapo tutaishi kwa taqwa litakuwa

**JUA LA TAQWA**

'Abdulqadir Jaylani alitoa nasaha zifuatazo kuhusiana na taqwa: "Ewe kijana, taqwa ndio muhimu, fanya kila juhudi upate taqwa ili roho yako iepushwe na uadui wa ndani na njia za uovu na hivyo irejee kwenye wema. Ewe kijana! Unapokusanya mali za dunia, usiwe kama yule anayekusanya kuni usiku, asiyejua nini anachokikusanya. Chukua tahadhari kubwa ili ufahamu kama vitu hivi vya dunia ni vya halali au haramu, na dumu na tauhiid na taqwa muda wote." Chimbuko la nasaha hizi lilikuwa ni dua hii aliyoomba Mtume kwa ajili ya taqwa

**"MWENYEZI MUNGU AKUJAALIE TAQWA"**

Mtu mmoja alikuja kwa Mtume na kusema, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, mimi nakwenda safarini. Naomba uni-

ombee dua!" Mtume, akasema, "Mwenyezi Mungu akujaalie taqwa." Kisha Mtu huyo akasema, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, niombee tena kidogo!" Mtume akajibu, "Mwenyezi Mungu akusamehe dhambi zako." Swahaba huyo akasema, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu niombee tena kidogo, naomba mama na baba yangu wawe fidia yako," Mbora wa viumbe hapo akasema, "Mwenyezi Mungu akujaalie wepesi popote unapotenda wema." (Tirmidhi, Da'awat, 44:3444).

Muradi wa dua hizi ulikuwa ni kubainisha umuhimu wa taqwa; kwanza Mtume alimuomba Mwenyezi Mungu awajaalie taqwa wale waliotaka kuombewa dua, kisha akawaombea msamaha wa dhambi zao na kisha akawaombea wepesi katika matendo mema. Sababu ya kuomba hivyo ilikuwa ni kwamba mambo haya huweza kutokea iwapo tu mtu ana taqwa moyoni; bila taqwa, dhambi hazitasamehewa wala matendo mema hayawezi kufanikiwa. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu anatutaka tuwe na taqwa na hututia katika mitihani ya taqwa katika matendo yetu na mambo yetu yote. Mtihani wa utii wetu, mahaba yetu na heshima yetu kwa Mtume unaitwa

**MTIHANI WA TAQWA**

Ifuatayo ni aya ya Qur'an: "Kwa hakika wale walioangusha sauti mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa kumuogopa Mwenyezi Mungu. Basi yatakuwa maghufira na thawabu kubwa. Wale wanaokwita nyuma ya nyumba, wengi wao hawafahamu (adabu)" (Hujurat, 49:3-4).

Hii ina maana kuwa adabu tuioneshayo mbele ya Mtume Muhammad (saw) kwamba tuige vitendo vyake na tufuate njia yake ya maisha na kwamba tumfahamu, yote hii ni mitihani

ya taqwa kwa ajili ya nafsi zetu. Ni neema kujenga mapenzi yetu kwake sanjari na kujikurubisha zaidi kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, taqwa katika matendo yetu ya kila siku kuanzia imani hadi matendo mema ndio inayopaswa kuwa vazi la nafsi zetu.

**VAZI LA TAQWA**

"Enyi wanaadamu! Hakika tumekuteremshieni nguo zifichazo tupu zenu na nguo za pambo; na nguo za uchaMungu ndizo bora." (A'raf, 7:26). Vazi au nguo za taqwa ndizo nguo hasa zilizopamba nafsi za Manabii na Marafiki wa Mwenyezi Mungu. Ifuatayo ni Hadith mashuhuri. Siku moja Imam Abu Hanifa alikuwa na kazi ya kusafisha doa dogo sana la uchafu katika nguo yake. Wachache miongoni mwa maswahaba wake, bila kuona ulazima wa jambo hilo, wakasema, "Ewe Imam, kwa mujibu wa tafsiri yako ya sharia ya Kiislamu, doa hili halikuzuilii kuswali, sasa kwa nini unapata tabu yote hiyo?" Imam akajibu, hiyo yaweza kuwa sheria ya Kiislamu lakini hii ni taqwa."

Kuishi maisha ya utii kwa Mwenyezi Mungu ni kuishi kwa mujibu wa aya ifuatayo ya Qur'an katika kila kipengele cha maisha: " Basi (ewe Mtume)! Endelea na uwongofu kama ulivyoamrishwa." (Hud, 11:112).

Mwenyezi Mungu sio tu ametutaka kufanya vitendo vizuri, bali pia anazingatia na kutazama kiwango chetu cha taqwa. Kwa hali hiyo, yawezekana kusema kuwa dini ndiyo uhai wa taqwa ambapo rehema na nusra ya Mwenyezi Mungu iko kwa waumini wanaojitahidi kupata radhi za Mwenyezi Mungu kwa taqwa ya kweli. Kheri yote ya Mwenyezi Mungu hapa duniani na Akhera inawahusu wale wenye taqwa (wam-

chao Mwenyezi Mungu). Hivyo basi, kuutakasa moyo na dhambi na uovu kwa njia ya taqwa ndiyo furaha ya kweli na ndiyo njia ya nusra kwa walimwengu. Masurufu yetu pekee ya imani ni

**MASURUFU YA TAQWA**

Kadri mapenzi na ilimu ya mtu juu ya Mwenyezi Mungu, vinavyoongezeka, ndivyo taqwa nayo inavyoongezeka na jambo hili ndilo litakiwalo kwetu, kwani taqwa ya moyoni ndiyo ifikayo kwa Mwenyezi Mungu kutokana na matendo yetu ya uchaMungu. Inabainishwa katika Qur'an kuwa "Nyama zao (wanyama hao wanaochinjwa) hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao, lakini inafika kwake Mwenyezi Mungu taqwa yenu." (Hajj, 22:37).

Rumi katutahadharisha juu ya ukweli huu, akisema: "Msithubutu kutoa kafara ya sisira la mbuzi!" Taqwa ya aina hii siyo ile inayotambuliwa na akili bali; ni ile inayohisika na kutimizika moyoni. Kuhusiana na hili, Mwenyezi Mungu kabainisha: "Je afanyae ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama na kuogopa Akhera na kutarajia rehema ya Mola wake (ni sawa na asiyefanya hayo?) Sema: "Je wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wasiojua?" Wanaotanabahi ni wale wenye akili." (Zumar, 39:9).

Sanjari na elimu hii, lazima:

1.Tumsujudie Mwenyezi Mungu nyakati za usiku.

2. Tusimame sawasawa katika ibada

3.Tujikinge na adhabu ya Akhera, (tusighafilike na maisha ya muda).

4. Tuombe rehema za Mwenyezi Mungu.

Ni maulamaa wenye sifa hizi tu ndio wenye sifa za kuheshimiwa. Undani wa ukweli huu unaelezwa katika Hadith hii: "Wale waongezao ilimu bila kuongeza taqwa yao, hujitenga mbali na Mwenyezi Mungu." Ndiyo maana Mwenyezi Mungu hatutaki kujiandaa na Akhera kwa masurufu ya vitu au kwa vitu vya kimaada. Masurufu ayatakayo kwetu ni masurufu ya taqwa. Ni sawa kabisa na kununua gari mpya halafu ukapuuza kutia mafuta, ndivyo elimu kavu nayo itakavyokosa manufaa katika safari ya kuyaelekea maisha ya milele.

Kama tunavyoweza kuona, taqwa ndiyo yenye umuhimu mkubwa kwa safari ya milele. Ndani ya Qur'an tunasoma, "Na chukueni masurufu (ya kutumia njiani). Na hakika masurufu bora ni yale yanayomfanya mtu asiombe. Na nicheni Mimi, enyi wenye akili." (Baqara, 2:197).

Ni faraja ilioje hii kwa wale wanaofunga safari ya kuyaendea maisha ya milele wakiwa na masurufu ya taqwa!

**Ewe Mwenyezi Mungu! Tujaalie masurufu ya taqwa-taqwa ya Manabii. Kwa kila muda wa maisha yetu, tujaalie taqwa iwe vazi la nafsi zetu milele na milele! Yahitimishe maisha yetu kwa furaha na tujumuishe katika Radhi na Kheri yako! Tujaalie afya na ijaalie taqwa yetu iwe masurufu katika njia ya kuyaendea maisha ya milele!**

Amin!

..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................

FOR FREE IN PDF FORMAT

# ISLAMIC WORKS

YOU CAN DOWNLOAD IN PDF FORMAT

**1350 BOOKS** IN **60 LANGUAGES** FOR FREE




Islamic books in different languages are waiting
for you in PDF format at the web site
www.islamicpublishing.org

ERKAM PUBLICATIONS | islamicpublishing.org